KUCHUNGUZA MATUMIZI YA MBINU ZA KISANAA NA DHAMIRA KATIKA TAMTHILIYA YA MORANI

ABDULHADI MOHAMED ABDULHADI ABOURWEESHAH

TASINIFU ILIYOWASILISHWA KWA AJILI YA KUTIMIZA SHARTI PEKEE LA KUTUNUKIWA SHAHADA YA UZAMILI YA KISWAHILI YA CHUO KIKUU HURIA CHA TANZANIA

2017

UTHIBITISHO

Aliyetia sahihi hapa anathibitisha kuwa amesoma tasinifu hii iitwayo ***Kuchunguza Matumizi ya Mbinu za Kisanaa na Dhamira katika Tamthiliya ya Morani,*** na anapendekeza ikubaliwe na Chuo Kikuu Huria Cha Tanzania kwa ajili ya kutimiza sharti pekee la kutunukiwa Digrii ya Uzamili (M.A) ya Kiswahili ya Chuo Kikuu Huria Cha Tanzania.

_____

Sheikh, Profesa, Daktari, T.S.Y.M. SENGO

(Msimamizi)

Tarehe: _____

HAKIMILIKI

Hairuhusiwi kuiga au kunakili kwa namna yoyote sehemu yoyote ile ya tasinifu hii kwa njia yoyote kama vile kielektroniki, kurudufu nakala, kurekodi au njia nyingine yoyote bila ya idhini ya mwandishi au ya Chuo Kikuu Huria cha Tanzania kwa niaba.

TAMKO

Mimi, **Abdulhadi Mohamed Abdulhadi Abourweeshah**, ninathibitisha kuwa, tasinifu hii ni kazi yangu halisi na haijawahi kuwasilishwa katika Chuo Kikuu kingine chochote kwa ajili ya kutunukiwa shahada nyingine yoyote.

Saini

Tarehe

TABARUKU

Kazi hii ninaitabaruku kwa wananchi wote wa Libya wanaopenda kujifunza lugha ya Kiswahili.

SHUKURANI

Ninapenda kutoa shukurani zangu za dhati kwa Mwenyezi Mungu mwingi wa rehema na mwenye kurehemu kwa kunijaalia afya njema katika kipindi chote cha masomo yangu. Pia, ninamshukuru kwa kuijaalia familia yangu salama na amani katika kipindi chote nikiwa katika nchi ya Tanzania kwa ajili ya kukamilisha masomo yangu. Kwa hakika hakuna apasaye kushukuriwa zaidi ya Mwenyezi Mungu na hivyo ninasema Alihamdulilahi Rabilaalamina.

Kipekee kabisa ninapenda kumshukuru mwalimu wangu Profesa Tigiti Shaban Yusuph Mnyagatwa Sengo kwa kunifundisha lugha ya Kiswahili pamoja na fasihi ya Kiswahili. Mwalimu wangu alinivumilia sana kutokana na uchanga wangu katika lugha ya Kiswahili ambapo kila mara nilipata taabu kutamka maneno ya Kiswahili kwa ufasaha lakini alirudia mara tena katika kunielekeza bila kuchoka. Ninakushukuru sana mwalimu wangu na Allah atakulipa mema yote uliyonifanyia.

Pia ninatoa shukurani zangu za dhati kwa serikali ya watu wa Libya kwa kunipatia fedha za masomo na kujikimu katika kipindi chote nilichokaa hapa Tanzania. Naisihi serikali yangu iendelee kuwasomesha wanafunzi wengine ili hatimaye kuwe na wataalamu wengi wa lugha ya Kiswahili katika nchi ya Libya.

IKISIRI

Lengo kuu la utafiti huu lilikuwa ni kuchunguza matumizi ya mbinu za kisanaa katika tamthiliya ya *Morani*. Ili kutimiza lengo hili kuu tulikuwa na malengo mahususi matatu; kuchambua matumizi ya mbinu za kisanaa za tamathali za usemi katika tamthiliya ya *Morani*, kuelezea matumizi ya mbinu za kisanaa zisizo tamathali za usemi katika tamthiliya ya *Morani* na kubainisha dhamira zitokanazo na matumizi ya mbinu za kisanaa katika tamthiliya ya *Morani*. Data za utafiti zilikusanywa kwa kutumia mbinu za usomaji makini na upitiaji wa nyaraka. Uchambuzi wa data umefanywa kwa kutumia mbinu ya mkabala wa kimaelezo na nadharia za Simiotiki na Korasi. Malengo mahususi matatu ya utafiti huu yalitimizwa vizuri ambapo kwa upande wa mbinu za kisanaa za tamathali za usemi tumechambua tamathali nne ambazo ni tashibiha, mbalagha, takriri na usambamba. Mbinu za kisanaa zisizo tamathali za usemi ni matumizi ya wahusika, wimbo, wahusika wa kikorasi na motifu. Kwa upande wa dhamira zitokanazo na matumizi ya mbinu za kisanaa tumebaini dhamira za uongozi na uhujumu uchumi, ugumu wa maisha, matabaka na haki na usawa.

YALIYOMO

UTHIBITISHO ..... **ii**

HAKIMILIKI ..... **iii**

TAMKO ..... **iv**

TABARUKU ..... **v**

SHUKURANI ..... **vi**

IKISIRI ..... **vii**

SURA YA KWANZA **1**

1.0 UTANGULIZI **1**

1.1 Utangulizi wa Jumla **1**

1.2 Usuli wa Tatizo la Utafiti **2**

1.3 Tatizo la Utafiti **6**

1.4 Malengo ya Utafiti **6**

1.4.1 Lengo Kuu la Utafiti **7**

1.4.2 Malengo Mahususi **7**

1.5 Maswali ya Utafiti **7**

1.6 Umuhimu wa Utafiti **7**

1.7 Mipaka ya Utafiti **8**

1.8 Vikwazo vya Utafiti na Utatuzi Wake **9**

1.9 Mpangilio wa Tasinifu **9**

SURA YA PILI **11**

2.0 MAPITIO YA KAZI TANGULIZI NA MKABALA WA KINADHARIA **11**

2.1 Utangulizi **11**

2.2 Utafiti wa Fani ya Tamthiliya **11**

2.3 Utafiti wa Maudhui katika Tamthiliya **13**

2.4 Utafiti kuhusu Tamthiliya ya Morani **16**

2.5 Mkabala wa Kinadharia **19**

2.5.1 Nadharia ya Simiotiki **19**

2.5.2 Nadharia ya Korasi **23**

2.6 Hitimisho **24**

SURA YA TATU **25**

3.0 MBINU ZA UTAFITI **25**

3.1 Utangulizi **25**

3.2 Eneo la Utafiti **25**

3.3 Usanifu wa Utafiti **26**

3.4 Kundi Lengwa **26**

3.5 Sampuli na Usampulishaji **27**

3.6 Data Zilizokusanywa **28**

3.6.1 Data za Msingi **28**

3.6.2 Data za Upili **28**

3.7 Mbinu za Kukusanyia Data **29**

3.7.1 Mbinu ya Usomaji Makini **29**

3.7.2 Upitiaji wa Nyaraka **29**

3.8 Mbinu za Kuchambua Data **30**

3.8.1 Mkabala wa Kimaelezo **30**

3.9 Usahihi wa Data **31**

3.10 Hitimisho **31**

SURA YA NNE **32**

4.0 UWASILISHAJI, UCHAMBUZI NA MJADALA WA DATA ZA UTAFITI **32**

4.1 Utangulizi **32**

4.2 Mbinu za Kisanaa za Tamathali za Semi katika Morani **32**

4.2.1 Tashibiha **33**

4.2.2 Mbalagha **36**

4.2.3 Takriri **40**

4.2.4 Usambamba **43**

4.3 Mbinu za Kisanaa Zisizo za Kitamathali katika Morani **45**

4.3.1 Matumizi ya Methali **46**

4.3.2 Matumizi ya Wimbo **49**

4.3.3 Wahusika wa Kikorasi **51**

4.3.4 Motifu ya Namba **54**

4.4 Dhamira katika Tamthiliya ya Morani **57**

4.4.1 Uongozi na Uhujumu Uchumi **57**

4.4.2 Maisha Magumu **62**

4.4.3 Matabaka **64**

4.4.4 Haki na Usawa **66**

4.5 Hitimisho **67**

SURA YA TANO **69**

5.0 HITIMISHO, MUHTASRI NA MAPENDEKEZO **69**

5.1 Utangulizi **69**

5.2 Muhtasari **69**

5.2.1 Mbinu za Tamathali za Usemi 69

5.2.2 Mbinu za Kisanaa Zisizo za Kitamathali 71

5.2.3 Dhamira katika Morani 72

5.3 Hitimisho 72

5.4 Mapendekezo 73

MAREJELEO 74

SURA YA KWANZA

1.0 UTANGULIZI

1.1 Utangulizi wa Jumla

Tasinifu hii inahusu kuchungunza mbinu za kisanaa na dhamira katika tamthiliya ya *Morani*. *Morani* ni tamthiliya iliyoandikwa na Emmanuel Mbogo ambaye ni profesa aliyebobea katika fani ya tamthiliya na filamu. Tamthiliya hii iliandikwa mwaka 1993 ikiwa na dhamira kuu inayohusu uhujumu uchumi. Uhujumu uchumi ni tatizo kubwa ambalo liliikabili serikali ya awamu ya kwanza chini ya utawala wa Mwalimu Julius Kambarage Nyerere. Uhujumu uchumi ni kitendo cha baadhi ya watu hasa wale wenye mamlaka na madaraka kutumia mamlaka waliyonayo kujinufaisha na mali za umma kinyume na sheria na taratibu zilizowekwa. Katika maisha ya leo, uhujumu uchumi ndio huo unaoitwa ufisadi na rushwa.

Kimsingi, katika kipindi cha utawala wa mwalimu Julius Kambarage Nyerere kulikuwa na waziri mkuu aliyeitwa Edward Moringe Sokoine aliyepambana vikali na wahujumu uchumi. Kiongozi huyo alikuwa shujaa ambaye hakumuogopa mhujumu uchumi yeyote yule na wala hakurudishwa nyuma na mtu yeyote katika kuwashughulikia wahujumu uchumi. Tamthiliya ya Morani inasawiri jitihada hizo za kiongozi huyo katika kupambana na uhujumu uchumi. Jina la tamthiliya hii ni Morani ambalo hutumika kuwarejelea vijana wa Kimaasai walio katika umri wa kati ambao husifika kwa uwezo wao mkubwa wa kuua simba na kutembea umbali mrefu na wanyama kwa ajili ya kutafuta majani na maji. Maasai ni jamii ya kifugaji na mara nyingi hufuga mifugo yao katika maeneo ya porini yenye wanyama wakali

kama simba, chui na wengineo. Wanyama hao wakali huatarisha maisha ya mifugo lakini uwepo wa morani huiweka mifugo yote katika hali ya usalama. Hivyo basi, tamthiliya ya Morani ni istiara kumhusu kiongozi huyo shujaa katika nchi ya Tanzania ambaye alifariki kwa ajali ya gari mwaka 1984 mkoani Morogoro.

Tasinifu hii imechunguza matumizi ya mbinu za kisanaa na dhamira katika tamthiliya ya *Morani* ili kuweza kuonyesha ni mbinu zipi za kisanaa zimetumiwa na mwandishi katika kujenga dhamira. Tunaposema mbinu za kisanaa tuna maana ya ule ufundi wa kisanaa ambao unatumiwa na mwandishi wa kazi ya fasihi katika kuijenga kazi yake. Ufundi wa kisanaa hutegemea na matumizi ya mbinu za kisanaa ambazo mtunzi anazitumia katika kazi yake na mara nyingi humtofautisha na watunzi wengine. Kwa jumla, mbinu za kisanaa hupatikana ndani ya vipengele vya fani ya kazi ya fasihi ikiwa ni pamoja na matumizi ya lugha, wahusika, mandhari, mtindo na muundo. Matumizi ya mbinu za kisanaa yaliyotafitiwa katika tasinifu hii yanatokana na baadhi ya vipengele hivi vya fani kama ilivyowasilishwa katika sura ya nne.

1.2 Usuli wa Tatizo la Utafiti

Tamthiliya kwa maana ya jina si utanzu mkongwe katika fasihi ya Kiswahili ikilinganishwa na tanzu za hadithi, ushairi, semi na sanaa za maonyesho. Semzaba (2003) anaeleza kuwa utanzu wa tamthiliya ulianza kutumika kama moja ya tanzu za fasihi pale wakoloni walipoingia na kutawala nchi za Afrika ya Mashariki. Wakoloni hao ambao waliingiza michezo ya kuigiza katika mataifa waliyoyatawala kama fani ya kujiburudishia baada ya kazi. Tamthiliya walizozileta kwa mara ya kwanza

zilikuwa ni kwa ajili yao wao wenyewe na watu wa kawaida ambao ni wananchi hawakupata nafasi ya kutazama tamthiliya hizo (Mlama, 2003). Suala hili linakwenda sambamba na hali halisi ya maisha ilivyokuwa katika kipindi cha ukoloni kwani mwananchi alikuwa akifanya kazi za kumzalishia mkoloni muda wote na hivyo asingeweza kupata muda wa kutazama au kusoma tamthiliya hizo zilizoletwa na wakoloni. Pia, katika kipindi hicho cha ukoloni, wananchi walitazamwa kama watu duni ambao si wastaarabu na hawana hadhi ya kutazama tamthiliya za Kizungu (Mugambi, 1982).

Maelezo ya Semzaba (2003) na Mlama (2003) ni sahihi katika kufafanua namna utanzu wa tamthiliya ulivyoingia na kuanza kutumika kama utanzu wa fasihi ya Kiswahili. Hata hivyo, haina maana kuwa, fasihi ya Kiswahili haikuwa na utanzu kama huo bali ni tofauti chache tu zilikuwepo kati ya tamthiliya na sanaa za maonyesho. Sanaa za maonyesho ni utanzu wa fasihi simulizi ambao unahusisha vitendo vya uigizaji wa kisanaa kwa lengo la kuwasilisha dhamira kwa hadhira iliyokusudiwa. Utanzu huu una vipera vidogovidogo kama vile maigizo, majigambo, vichekesho, michezo ya watoto, ngoma na matambiko (Masoud, 2013). Utanzu huu umekuwepo katika jamii ya Waswahili, Watanzania na Waafrika kwa miaka mingi kabla ya ujio wa wageni. Tofauti na tamthiliya, sanaa za maonesho hazikuwa zimeandikwa na hivyo kuwasilishwa kwa njia ya mdomo tu (Kiango, 1992).

Baada ya muda kupita na Watanzania na Waafrika kujifunza kusoma na kuandika walianza kuandika tamthiliya za Kiswahili kutokana na misingi ya tamthiliya za Kizungu zilizofuata kanuni za Kiaristoto (King’ei, 1987). Watunzi maarufu

walioandika tamthiliya nyingi za Kiswahili ni Ebrahim Hussein, Penina Mlama, Said Ahmed Mohamed na Emmanuel Mbogo. Kutokana na watunzi hawa kuandika kazi nyingi za tamthiliya wapo wahakiki na wanafasihi ambao wamevutiwa katika kutafiti fani na maudhui katika tamthiliya hizo za watunzi hawa na wengine ambao sikuwataja hapa. Ligembe (1995) ni mmoja kati ya wataalamu aliyetafiti matumizi ya sitiari katika tamthiliya ya *Lina Ubani* iliyoandikwa na Penina Mlama.

Mtafiti huyu alibaini kuwa mtunzi wa *Lina Ubani* amejenga sitiari kwa kutumia vitu na mambo yayopatikana katika mazingira halisi ya jamii. Hii imesaidia tamthiliya hiyo kuakisi maisha halisi ya jamii kwa kuipatia maudhui yanayoilenga jamii. Utafiti huu umetusaidia kupata mwanga wa namna ya kushughulikia mbinu za kisanaa katika tamthiliya ya *Morani* kwani sitiari ni moja kati ya vipengele vya kifani kinachotumika katika kuunda maudhui ya kazi ya fasihi.

Mugambi (1982) alichunguza maudhui ya tamthiliya za Kenya zilizoandikwa tangu mwaka 1957 mpaka 1981 na kuchanganua maudhui ya aina tofautitofauti. Maudhui hayo ni udhalimu, usaliti, ukombozi, nafasi ya mwanamke katika jamii, utetezi wa haki za wanyonge, ubepari na ukoloni mamboleo. Uchanganuzi huu wa maudhui katika tamthiliya za Kenya umetusaidia kufahamu mbinu za kisanaa zilizotumiwa na waandishi wa kazi hizo katika kuibua dhamira hizi. Tulipokuwa tukiisoma kazi hii ya Mugambi (1982) tulibaini kuwa mbinu za kisanaa kama vile lugha ya tamathali za semi imetumika kwa kiasi kikubwa kuibua dhamira ndani ya tamthiliya hizo. Katika utafiti wetu tumetumia maarifa tuliyoyapata katika kusoma kazi ya Mugambi kuweza kuibua matumizi ya mbinu za kisanaa na dhamira katika tamthiliya ya *Morani*.

Mosoti (1993) alihakiki maudhui katika tamthiliya nne za Emmanuel Mbogo za *Giza Limeingia* (1980), *Tone la Mwisho* (1981), *Watoto Wetu* (1981) na *Ngoma ya Ng'wanamalundi* (1988). Maudhui yaliyobainishwa kutoka katika tamthiliya hizi ni ukombozi, dhuluma, usaliti, ubinafsi, na nafasi ya mwanamke katika jamii. Ingawa uchambuzi huu haukuhusisha tamthiliya ya *Morani* lakini umetusaidia katika kutambua dhamira zinazojitokeza katika tamthiliya za Emmanuel Mbogo na hivyo kutuwia rahisi kuchambua mbinu za kisanaa pamoja na dhamira katika tamthiliya ya *Morani*.

Naye Ramadhani (1995) alifanya utafiti linganishi wa tamthiliya za *Mashetani* na *Ngoma ya Ng'wanamalundi* za watunzi Ebrahim Hussein na Emmanuel Mbogo mtawalia. Katika utafiti huu aligundua kwamba watunzi hawa wawili wamefanana zaidi katika matumizi ya mbinu za kiuhalisia mazingaombwe kuibulia dhamira za kazi zao. Watunzi hawa ni mabingwa wa kutumia mbinu za kimiujizaujiza kuelezea masuala muhimu kama vile unyonyaji, utabaka, dhuluma, ufisadi, rushwa na ukandamizaji wa aina yoyote ile. Kazi ya Ramadhani ilitujengea uelewa kwamba, masuala ya kimiujizaujiza yanayotumiwa na waandishi hawa wawili katika kazi zao si ya kupuuzwa hata kidogo bali yanapaswa kutazamwa kwa macho yote mawili kwani ndani mwake ndimo mna maudhui na dhamira. Ingawa kazi hii haikuwa inahusiana na kuchunguza mbinu za kisanaa katika tamthiliya ya *Morani* lakini imetupatia ufahamu kwamba hata matumizi ya mbinu za kimiujizaujiza ni moja kati ya mbinu za kisanaa zitumikazo katika kazi za fasihi.

Kwa hakika, tukitazama maelezo haya ya kiusuli tunabaini tamthiliya za Kiswahili

zipo tena nyingi tu, na wahakiki na watafiti kadhaa wamejitokeza katika kufanya uchambuzi wa fani na maudhui katika tamthiliya hizo. Hata hivyo, hakuna mtafiti ambaye ametazama matumizi ya mbinu za kisana na dhamira katika tamthiliya ya *Morani* kwa umahususi. Hili ni pengo la maarifa ambalo utafiti huu umelishughulikia kwa kuchunguza matumizi ya mbinu za kisanaa katika tamthiliya ya *Morani* ya Emmanuel Mbogo.

1.3 Tatizo la Utafiti

Tamthiliya ya *Morani* ya mwandishi Emmanuel Mbogo ni moja kati ya tamthiliya zilizopata umaarufu mkubwa katika fasihi ya Kiswahili kutokana na kuelezea maudhui yenye uhalisia katika jamii. Matumizi ya mbinu za kisanaa katika kazi ya fasihi ndiyo hasa yanayosaidia katika kujenga na kuwasilisha vizuri dhamira kwa hadhira iliyolengwa. Katika utafiti huu tunataka kufahamu katika tamthiliya ya *Morani* kunatumiwa mbinu gani za kisanaa? Mbinu hizo zinatumika kuwasilisha dhamira gani? Tumejiuliza maswali haya kwa sababu tunafahamu kuwa kupambana na uhujumu uchumi ni kitu hatari kwa maisha ya mwandishi lakini yeye akaamua kuelezea suala hilo. Kukamilika kwa utafiti huu kumetoa mchango wa kitaaluma kuhusu mbinu za kisanaa ambazo zinaweza kutumika katika kuelezea masuala ambayo ni hatari katika jamii na hivyo wanafasihi watajifunza na kuzitumia katika maandishi yao.

1.4 Malengo ya Utafiti

Utafiti wa kitaalamu kama huu hufanywa kwa mtafiti kuwa na malengo maalumu ambayo anataka kuyafikia. Utafiti wetu ulikuwa na lengo kuu moja na malengo

mahususi matatu.

1.4.1 Lengo Kuu la Utafiti

Lengo kuu la utafiti huu lilikuwa ni kuchunguza matumizi ya mbinu za kisanaa katika tamthiliya ya *Morani*.

1.4.2 Malengo Mahususi

(i) Kuchambua matumizi ya mbinu za kisanaa za tamathali za usemi katika tamthiliya ya *Morani*.

(ii) Kuelezea matumizi ya mbinu za kisanaa zisizo tamathali za usemi katika tamthiliya ya *Morani*.

(iii) Kubainisha dhamira zitokanazo za matumizi ya mbinu za kisanaa katika tamthiliya ya *Morani*.

1.5 Maswali ya Utafiti

(i) Ni mbinu zipi za kisanaa za tamathali za usemi zilizotumika katika tamthiliya ya *Morani*?

(ii) Ni mbinu zipi za kisanaa zisizo tamathali za usemi zilizotumika katika tamthiliya ya *Morani*?

(iii) Ni dhamira zipi zitokanazo na matumizi ya mbinu za kisanaa katika tamthiliya ya *Morani*?

1.6 Umuhimu wa Utafiti

Utafiti huu utakuwa na umuhimu mkubwa katika kuwafahamisha watunzi wa kazi za fasihi namna ya kutumia mbinu za kisanaa katika kuelezea masuala ambayo ni hatari

kwa maisha ya mtunzi kuyaelezea. Utafiti huu umechunguza mbinu za kisanaa zilizotumika kuelezea maudhui yanayohusiana na uhujumu uchumi ambao hufanywa na viongozi na watu wenye fedha nyingi wenye uwezo wa kununua haki na kuipindisha. Katika mazingira kama hayo maisha ya mtunzi yanaweza kuwa mashakani. Hata hivyo, kwa matumizi ya mbinu za kisanaa yaliyo makini mtunzi hukwepa rungu la wahusika hao wa uhujumu uchumi.

Utafiti huu pia utasaidia kuleta maarifa mpya ya kujaza pengo la maarifa lililokuwepo kutokana na kutotafitiwa kwa matumizi ya mbinu za kisanaa katika tamthiliya ya *Morani*. Kwa kufanya hivyo, utafiti huu utakuwa rejeleo muhimu kwa watafiti, wahakiki, walimu, wahadhiri na wanafunzi wa fasihi ya Kiswahili. Kutokana na utafiti huu wanaweza kupata mawazo mapya ya kutafiti katika tamthiliya na hatimaye kuongeza maarifa zaidi.

Utafiti huu pia utakuwa na umuhimu kwa watungaji wa sera zinazohusiana na mapambano dhidi ya uhujumu uchumi, rushwa na ufisadi. Katika tamthiliya ya *Morani* kunaelezwa namna rushwa inavyofanyika, viashiria vyake na jitihada zinazofanywa na vyombo husika katika kupambana na rushwa. Hivyo, vyombo vya kupambana na uhujumu uchumi, rushwa na ufisadi watakoposoma utafiti huu watapata mambo ya kuongeza katika sera na sheria za kupambana na vitendo hivi ambavyo ni adui wa maendeleo.

1.7 Mipaka ya Utafiti

Mwandishi Emmanuel Mbogo ni mmoja kati ya waandishi walioandika kazi nyingi za tamthiliya za Kiswahili katika ukanda wa Afrika ya Mashariki, Afrika na

Ulimwenguni kote. Miongoni mwa kazi alizoziandika ni *Giza Limeingia*, *Tone la Mwisho*, *Watoto Wetu*, *Ngoma ya Ng'wanamalundi*, *Morani*, *Fumo Liongo*, *Sundiata*, *Nyerere* na *Safari ya Kanaani*, *Mathai Wangari* na *Tom Mboya* kuzitaja baadhi tu. Katika utafiti huu tumetafiti tamthiliya ya *Morani* peke yake kwa kuwa tuliona kuwa inatosha katika kutupatia data tulizozihitaji katika utafiti huu. Katika tamthiliya hii tumechambua mbinu nne za kisanaa za tamathali za semi na mbinu nne za kisanaa sizizo tamathali za usemi na baada ya hapo tukabainisha dhamira nne zilizowasilishwa kutokana na matumizi ya mbinu za kisanaa katika tamthiliya ya *Morani*.

1.8 Vikwazo vya Utafiti na Utatuzi Wake

Uzungumzaji wa lugha ya Kiswahili kwa ufasaha ndiyo iliyokuwa changamoto kubwa katika kufanya utafiti huu. Mimi ni mzaliwa wa Libya ninayetumia Kiarabu kama lugha yangu ya kwanza na hivyo katika lugha ya Kiswahili mimi ni mwanafunzi. Mara kwa mara nilipoandika kazi yangu nimekuwa nikiandika kwa makosa kutokana na kutokujua lugha ya Kiswahili.

Katika kutatua kikwazo hiki, msimamizi wangu alinisaidia kupata mtafiti msaidizi ambaye alinisadia katika kujifunza lugha ya Kiswahili na masuala ya utafiti. Msaidizi huyu alikuwa ni mzaliwa wa Zanzibar na lugha yake ya kwanza ni Kiswahili.

1.9 Mpangilio wa Tasinifu

Tasinifu ya utafiti huu ina jumla ya sura tano zenye maudhui yanayotofautiana lakini shikamani katika kutimiza lengo kuu la utafiti. Sura ya kwanza inahusu utangulizi wa

utafiti ambapo vipengele kama vile usuli wa tatizo la utafiti, tatizo la utafiti, malengo ya utafiti na maswali ya utafiti vimewasilishwa. Vipengele vingine ni umuhimu wa utafiti, mipaka ya utafiti, vikwazo vya utafiti na utatuzi wake na mpangilio wa tasinifu. Sura ya pili inahusu mapitio ya kazi tangulizi na mkabala wa kinadharia. Sura ya tatu inahusu mbinu za kukusanya na kuchambua data za utafiti. Sura ya tano inahusu uwasilishaji, uchambuzi na mjadala wa data za utafiti huku sura ya mwisho ambayo ni ya tano ikiwasilisha hitimisho, muhtasari na mapendekezo.

SURA YA PILI

2.0 MAPITIO YA KAZI TANGULIZI NA MKABALA WA KINADHARIA

2.1 Utangulizi

Mapitio ya kazi tangulizi hufanywa kwa lengo la kupata uelewa mpana wa kipi kimefanyika na kipi hakijafanyika kuhusiana na mada ya utafiti. Sura hii ndiyo inayotoa uhakika wa kile kinachotafitiwa kuwa kimetafitiwa kwa kiasi gani na kumfanya mtafiti asirudie kitu ambacho tayari kimekwishafanyiwa utafiti. Ikiwa ipo kazi ambayo tayari imefanywa na inafanana na kazi ya sasa lakini mtafiti hakuwahi kuiona kazi hiyo bado kazi yake itakuwa ni tofauti na hiyo ya kwanza kwa sababu hajawahi kuiona. Katika sura hii tumewasilisha kazi tangulizi kayika mada ya utafiti katika fani ya tamthiliya na maudhui katika tamthiliya.

2.2 Utafiti wa Fani ya Tamthiliya

Utafiti kuhusu fani ya tamthiliya umefanywa na watafiti kadhaa wakichunguza vipengele mbalimbali vya fani. Fani huelezwa kama ufundi wa kisanaa unaotumiwa na mwandishi katika kuwasilisha maudhui ya kazi yake anayoiandika. Hii ni sawa na kusema kuwa fani ni chombo cha kubebea maudhui na kwa hiyo kuna uhusiano wa moja kwa moja baina ya fani na maudhui. Fani pekee wala maudhui pekee hayawezi kutengeneza kazi ya fasihi bali kwa upamoja wake. Ligembe (1995) alifanya utafiti na kuandika tasinifu ya uzamili kuhusu matumizi ya sitiari katika tamthiliya ya *Lina Ubani*. Katika utafiti huu ameainisha aina anuai za sitiari kama vile sitiari zenye kuonekana, sitiari zisizoonekana, sitiari za kuhisi na sitiari za kimlinganisho. Utafiti wa Ligembe (1995) umefungua uelewa wetu kuhusu matumizi ya mbinu za kisanaa

katika tamthiliya na tuliyahaulisha mawazo haya katika utafiti wetu. Ingawa utafiti wake haukuhusu tamthiliya ya *Morani* lakini hata katika *Morani* kuna matumizi ya tamathali za usemi zenye kulinganisha vitu viwili au zaidi vyenye sifa na tabia tofauti kufanana bila ya kuwa na tofauti.

Musyoka (1996) alifanya utafiti wa kuhakiki fani katika tamthiliya za *Uasi* (1980), *Malimwengu Ulimwengu* (1983) na *Tazama Mbele* (1987). Mtafiti alifanikiwa kubainisha matumizi ya vipengele mbalimbali vya fani kama mtindo, muundo, mandhari, matumizi ya lugha na wahusika. Tukirejelea kipengele cha matumizi ya lugha, mtafiti huyu alibaini kuwa matumizi ya tamathali za usemi yanajitokeza kwa kiasi kikubwa katika tamthiliya hizo ikilinganishwa na vipengele vingine vya lugha na vya fani kwa jumla. Mawazo haya ni sahihi tunayaunga mkono kwani lugha ndicho chombo cha kubebea maudhui na hivyo ni lazima kitawale katika kazi ya fasihi. Pia, unapozungumza juu ya matumizi ya lugha katika kazi ya fasihi, zaidi ya asilimia 80 unazungumza juu ya tamathali za usemi. Hii ni kwa sababu tamathali za usemi ni nyingi na hivyo ni lazima zijitokeze kwa kiasi kikubwa katika kazi ya fasihi. Uelewa huu tuliuchukuwa na kufanyia kazi katika utafiti huu hata tukafikia uamuzi wa kuwa lengo mahususi moja linzlohusiana na tamathali za usemi katika tamthiliya ya *Morani*.

Hata hivyo, utafiti wa Musyoka (1996) ulikuwa mpana sana kutokana na kuchunguza vipengele mbalimbali vya fani katika tamthiliya alizoziteua. Utafiti kama huu hauwezi kushughulikia jambo kwa mapana na mawanda zaidi kama utafiti ambao unashughulikia jambo moja. Mtafiti hawezi kupata muda na nafasi ya kushughulikia

jambo au kipengele kimoja kwa undani zaidi kwa sababu anahitajika kutoa maelezo kwa vipengele vingi. Utafiti wetu ulijikita katika kuchunguza mbinu za kisanaa kwa kuteua tamathali nne za semi, vipengele visivyo vya kitamathali navyo vinne na dhamira nne kutoka katika tamthiliya ya *Morani*. Vipengele hivi vimeelezwa kwa kina katika utafiti huu na kufanikiwa kutimiza lengo kuu la utafiti.

Mangare (2002) alifanya uhakiki wa tamthiliya ya *Amezidi* (1995) iliyoandikwa na Said Ahmed Mohamed akichunguza ni kwa vipi tamthiliya hii ni ya kibwege. Katika kutimiza lengo lake alizamia vipengele vya wahusika na uhusika, matumizi ya lugha na ploti. Katika utafiti huu ilibainika kwamba *Amezidi* ni tamthiliya ya kibwege ambapo wahusika wake kama akina Ame na Zidi wamethibitisha hilo. Hawa ni wahusika ambao wanaonyesha kukata tamaa katika maisha na kuyaona maisha kama kitu kisichokuwa na maana yoyote. Wahusika hawa wanakata tamaa ya maisha kutokana na hali ngumu ya maisha wanayokumbana nayo. Wahusika hawa wamesaidia kujenga dhamira ya kuwaelimisha watu juu ya namna ya kukabiliana na maisha kwa kujipanga na kutokukurupuka katika kuyaingia maisha. Maelezo ya Mangare (2002) tumeyachukuwa na kuyafanyia kazi katika utafiti ambapo sisi tumechunguza matumizi ya mbinu za kisanaa na dhamira katika tamthiliya ya *Morani*.

2.3 Utafiti wa Maudhui katika Tamthiliya

Maudhui ni jumla ya mambo yote ambayo mtunzi wa kazi ya fasihi anataka hadhira yake iyafahamu. Maudhui hujumuisha vipengele vya dhamira, falsafa, ujumbe, migogoro, msimamo wa mwandishi na maadili. Tamthiliya kama zilivyo kazi

nyingine za fasihi huwasilisha maudhui kupitia vipengele hivi kwa hadhira iliyokusudiwa. Watafiti kadhaa wamechunguza maudhui katika tamthiliya za Kiswahili ambapo Mugambi (1982) ndiye anayeanzisha ukurasa huu. Mtaalamu huyu alifanya utafiti uliolenga kuchunguza maudhui katika tamthiliya za Kenya zilizoandikwa tangu mwaka 1957 mpaka 1981 ambapo alibaini kuwa tamthiliya hizo zina maudhui kuntu ya kuifaa jamii. Maudhui hayo ni udhalimu, usaliti, ukombozi, nafasi ya mwanamke katika jamii, utetezi wa haki za wanyonge, ubepari na ukoloni mamboleo. Dhamira hizi ni mardudi kwani hata katika tamthiliya ya *Morani* pia zinajitokeza. Maelezo ya Mugambi yamekuza ufahamu wetu kuhusu dhamira katika tamthiliya na kutufanya kujiamini katika kuchunguza mbinu za kisanaa katika tamthiliya ya *Morani* na baadae kubainisha dhamira.

Naye Mosoti (1993) alihakiki maudhui katika tamthiliya nne za Emmanuel Mbogo za *Giza limeingia*, *Tone la Mwisho*, *Watoto Wetu* na *Ngoma ya Ng'wanamalundi*. Maudhui yahusianayo na dhamira za ukombozi, dhuluma, usaliti, ubinafsi na nafasi ya mwanamke katika jamii zimejitokeza katika tamthiliya hizo nne. Utafiti wa Mosoti (1993) ulihusisha tamthiliya za mwandishi Emmanuel Mbogo ambaye nasi tunatafiti tamthiliya yake ya *Morani*. Kazi ya Mosoti imepanuwa uelewa wetu kuhusu dhamira zinazopatikana katika kazi za Emmanuel Mbogo na kwamba hata *Morani* haiendi mbali na tamthiliya hizo nyingine kimaudhui na kidhamira. Utafiti wa Mosoti umetusaidia kuufanya utafiti wetu kuwa rahisi katika kukamilisha lengo mahususi la tatu lililokuwa limelenga kubainisha dhamira zinazojengwa na matumizi ya lugha ya kisanaa katika tamthiliya ya *Morani*.

Naye Sarara (1997) alitafiti maudhui katika tamthiliya za Said Ahmed Mohamed za *Pungwa* (1998), *Kivuli Kinaishi* (1990) na *Amezidi* (1995). Katika utafiti huu alibaini kuwa mwandishi amewasilisha dhamira za kudhulumiwa kwa mwanamke, mapambano ili kuleta ukombozi, ufisadi na uozo katika jamii. Utafiti wa Sarara ulikuwa na manufaa makubwa kwetu kutokana na namna alivyofanikiwa kuzipata dhamira hizo tulizozitaja. Ukitazama madondoo aliyoyatoa unabaini kwamba mtunzi alikuwa na ujuzi mkubwa kufahamu matumizi ya mbinu za kisanaa kama vile tamathali za usemi zinavyotumika katika kuibua dhamira. Katika utafiti wetu tumekuwa makini katika kutazama namna mbinu za kisanaa zilivyotumiwa na mwandishi katika kuwasilisha dhamira kwa hadhira iliyokusudiwa katika tamthiliya ya *Morani*.

Njogu na Chimerah (1999) walifanya utafiti na kuandika kitabu maarufu cha fasihi ya Kiswahili kinachoitwa *Ufundishaji wa Fasihi Nadharia na Mbinu*. Katika kitabu hicho kuna sura maalumu inayohusiana na ufundishaji wa tamthiliya. Tamthiliya zilizochambuliwa kama mfano wa kufundishia ni *Mashetani* ambayo inatajwa kuwa ni tamthiliya ya mivutano ya kiuchumi na *Amezidi* inayotajwa kuwa ni tamthiliya ya kibwege. Uchambuzi walioufanya tunakubaliana nao kwa asilimia mia moja na kuwa tamthiliya ya *Mashetani* inaelezea mivutano ya kiuchumi baina ya waliokuwa wakoloni na mataifa ambayo hapo awali yalitawaliwa. Uchambuzi walioufanya umetupatia mwanga wa namna dhamira zinavyojengwa na watunzi wa kazi za fasihi kwani kwa kupitia mhusika shetani wamebainisha mengi. Hii imeufanya utafiti wetu kuwa kazi nyepesi ambapo tumeweza kuchambua mbinu za kisanaa na dhamira katika tamthiliya ya *Morani*.

Masoud (2013) alifanya utafiti linganishi wa fani na maudhui katika tamthiliya za *Mashetani* na *Kivuli Kinaishi*. Katika utafiti huu anabainisha kuwa dhamira za ukombozi, utabaka, rushwa, nafasi ya mwanamke katika jamii na ukoloni mamboleo zinajitokeza katika tamthiliya hizo. Tunakubaliana na malezo ya Masoud (2013) kuwa tamthiliya hizi mbili ni tamthiliya za kiukombozi na dhamira zote alizoeleza kuwa zinasawiriwa katika tamthiliya hizo zinalenga katika kumkomboa mwanajamii kutoka katika dhuluma ifanywayo na viongozi dhidi ya watu wao. Maelezo haya tumeyachukuwa na kuoanisha na tamthiliya ya *Morani* na kugundua kuwa hata *Morani* ni tamthiliya ya kiukombozi ambapo ililengwa kuikomboa jamii kutoka katika mikono ya wahujumu uchumi. Wahujumu uchumi ni watu ambao wananufaika na rasilimali za nchi kwa masilahi yao binafsi na si ya wananchi wote. Kazi ya Masoud (2013) imeufanya utafiti wetu kuwa mwepesi kutokana na kudokeza maudhui ambayo pia yanapatikana katika *Morani* na kwa kuzitafiti mbinu za kisanaa katika tamthiliya hii tumeweza kubainisha dhamira kadhaa.

2.4 Utafiti kuhusu Tamthiliya ya Morani

Utafiti kuhusu tamthiliya ya *Morani* umefanywa na watafiti kadhaa wakiwa na malengo mbalimbali. Njogu na Chimerah (1999) ni miongoni mwa wanataaluma ambao wameielezea tamthiliya ya Morani. Katika kitabu chao maarufu cha ufundishaji wa fasihi wanaeleza kuwa Morani ni moja kati ya tamthiliya ambazo zimeundwa kwa fani nzuri na pia maudhui yake yana mafunzo mazuri kwa jamii. Maelezo haya ni sahihi ndiyo maana hata mtaala wa shule za sekondari kidato cha tano na sita unawataka wanafunzi wanaosoma Kiswahili kukisoma kitabu hicho. Kuteuliwa kwa kitabu kutumika kama kitabu cha kiada kama ilivyo *Morani* ni ishara

kuwa kitabu hicho kinakidhi vigezo vyote vya ubora unaotakiwa. Maelezo haya kwa hakika yanetuchochea kufanya utafiti huu ili kuweza kubainisha matumizi ya mbinu za kisanaa na dhamira zilizopo katika tamthiliya ya *Morani*.

Naye Wafula (1999) aliandika kitabu kuhusu maendeleo ya tamthilkiya ya Kiswahili na kueleza mambo mbalimbali akirejelea tamthiliya za Kiswahili. Miongoni mwa tamthiliya alizozirejelea ni pamoja na *Morani* ya Emmanuel Mbogo ambapo anaitaja kuwa ni tamthiliya ya kimajaribio. Ni tamthiliya ya kimajaribio kwa sababu ina vipengele vya kimajaribio kama wahusika, kuchanganya tanzu, matumizi ya lugha ya mafumbo, tamathali za usemi, marudiorudio na mwingingiliano wa tanzu kuzitaja kwa uchache. Maelezo haya tunakubaliana nayo kwa sababu tamthiliya ya *Morani* imeandikwa katika kipindi ambacho wanazuoni wa Kiafrika walitaka kuleta mapinduzi katika uandishi wao wa kazi za fasihi ili ziendane na mazingira halisi ya jamii. Hivyo, tamthiliya hii ni mfano mzuri wa mapinduzi hayo ambayo yamesaidia katika kujenga umbo la tamthiliya yenye asili ya Afrika tofauti za wakoloni ambazo zilionekana kuwa ni bora kuliko za Waafrika. Mawazao haya yametusaidia kufahamu baadhi ya vipengele vya kisanaa vinavyopatikana katika tamthiliya ya *Morani* na sisi tumeviwasilisha kwa mawanda zaidi kuliko alivyofanya Wafula (1999).

Wamitila (2002) aliandika kitabu kuhusu vipengele vya uhakiki katika fasihi na kurejelea tanzu mbalimbali ukiwemo utanzu wa tamthiliya. Tamthiliya ya *Morani* ni moja kati ya kazi zilizorejelewa ambapo inaelezwa kuwa dhamira kuu katika tamthiliya hii ni uhujumu uchumi ambao unasawiriwa kisanaa. Anaeleza kuwa katika

kupambana na uhujumu uchumi ni lazima tahadhari kubwa ichukuliwe ili kuepuka madhara yanayoweza kutokea. Tumeona katika tamthiliya ya Morani kuwa, mpambanaji mkuu dhidi ya uhujumu uchumi aliuawa kitu ambacho kinaonyesha kuwa mapambano dhidi ya uhujumu uchumi ni hatari sana. Maelezo haya tumeyachukua na kuyafanyia kazi katika tasinifu yetu ambapo kimsingi dhamira ya uhujumu uchumi pia tumeiwasilisha katika uchambuzi wa data za utafiti wetu. Tofauti na kazi ya Wamitila, utafiti wetu umeielezea dhamira hii kwa mapana zaidi.

Mutembei (2012) katika kitabu chake cha Korasi katika fasihi ameizungumzia tamthiliya ya *Morani* kuwa nayo inaweza kuchambuliwa kwa kutumia nadharia hiyo. Anaeleza kuwa ujenzi wa jina la kitabu umejengwa kikorasi ikiwa na maana kuwa yote yanayotokea ndani ya kitabu yanarejelea jina la kitabu ambalo ni *Morani*. Msomaji mzoefu wa kazi za fasihi anapokutana na jina hili la kitabu na anapoanza kusoma anabaini kuwa kila kitu kimechorwa kwa namna ambayo inaonyesha uhodari wa Morani kuwa ni shujaa ambaye huwa kaubali kushindwa na jambo hata kama linahatarisha usalama wake. Maelezo haya yametusaidia kupata ufahamu zaidi kuhusiana na namna nadharia ya Korasi inavyoweza kutumika katika kuchambua data za utafiti wetu. Tumeyatumia mawazo ya Mutembei katika kuchambua wahusika wa kikorasi na motifu ya namba katika tamthiliya ya *Morani*.

Maelezo na mawazo ya watafiti kuhusu tamthiliya ya *Morani* yanathibitisha kuwa tamthiliya hii ina utajiri mkubwa wa vipengele vya kisanaa ambavyo vinahitaji kufanyiwa utafiti mpana zaidi. Katika kazi hizi tulizopitia kwa mujibu wa ufahamu wetu zinaonyesha kuwa tamthiliya ya *Morani* haijafanyiwa utafiti wa kina kuhusiana

na matumizi ya mbinu za kisanaa kama ambavyo imekusudiwa kufanywa katika utafiti wetu. Hata hivyo, mawazo ya wataalamu hawa yametusaidia sana kupanua uelewa wetu kuhusu tamthiliya ya *Morani* na mawazo yao tumeyafanyia kazi katika tasinifu hii.

2.5 Mkabala wa Kinadharia

Nadharia kama inavyoelezawa na Kothari (2008) ni kanuni na taratibu inayoelezea namna kitu kilivyo au kinavyotakiwa kuwa. Katika jamii kila kitu hufanyika kwa kuzingatia nadharia fulani hata kama mfanyaji wa kitu hicho hakubainisha nadharia anayoitumia. Kwa mfano, katika shughuli ya biashara, kila mfanyabiashara hufanya biashara kwa kuzingatia nadharia fulani kwa lengo la kupata faida. Wapo wafanyabiashara ambao wanaongozwa na nadharia ya kuwa kukopesha bidhaa kwa wateja si jambo jema kwani huchangia kupata hasara na kupoteza wateja. Lakini wapo wafanyabiashara ambao huamini kuwa kuwakopesha wateja bidhaa ni njia ya kuongeza faida na kuongeza wateja. Hizi ni baadhi tu ya nadharia zinazowaongoza katika kufanya biashara. Utafiti wa fasihi kama huu wetu nao ni moja kati ya mambo ambayo hufanywa kwa kufuata muongozo wa nadharia. Nadharia za Simiotiki na Korasi ndizo zilizotumika katika kuongoza utafiti huu.

2.5.1 Nadharia ya Simiotiki

Simiotiki kama lilivyo jina lenyewe ni nadharia inayohusiana na lugha ya misimbo, picha na ishara inayotumika katika kazi za fasihi (Eco, 1976). Misingi ya nadharia hii inaeleza kuwa katika lugha huwa kunakuwa na vitu viwili ambavyo ni kitaja na kirejelee. Kitaja ni jina linalotaja kitu na kirejelee ni kile kinachotajwa na jina hilo.

Kwa mfano, jina “nyumba” ni kitaja ambacho hutumika kutaja mahali maalumu ambapo ni makazi ya uhakika ya mtu na familia yake. Katika hali ya kawaida huwa hakuna uhusiano wa moja kwa moja baina ya jina “nyumba” na kile kinachowakishwa na jina hilo. Hii inathibitishwa na ukweli kuwa kila jamii au kabila kuwa na jina lake linalotumiwa kuiita nyumba. Hata hivyo, kuna baadhi ya majina ambayo huwa na uhusiano wa moja kwa moja kati ya jina na kile kinachowasilishwa na jina hilo. Majina hayo ni yale yenye yanayotokana na mwigo wa sauti inayotolewa na kile kinachorejelewa. Majina kama hayo ni “nyau” ambalo humrejelea mnyama paka ambaye wakati anapolia hutoa sauti ya “nyau, nyau” ndio hapo akaitwa nyau.

Matumizi ya lugha ni ndiyo yanayoifanya fasihi kuwa tofauti na sanaa nyingine kwani malighafi ya kazi ya fasihi ni lugha (Cobley, 2001). Matumizi ya lugha katika kazi za fasihi huwa ni ya kisanaa na si lugha ya kawaida ambayo inatumika katika mawasiliano ya kila siku ya wanajamii. Lugha ya kifasihi ni ile iliyojaa matumizi ya mafumbo, picha, ishara, tanakali sauti, sitiari, tashibiha, tashihisi na tafsida. Ili mtafiti au mchambuzi wa kazi ya fasihi aweze kuchambua kazi ya fasihi kwa makini ni lazima atumie nadharia za uhakiki wa kifasihi kama nadharia hii ya Simiotiki. Kwa kuwa utafiti wetu unahusu kuchunguza matumizi ya mbinu za kisanaa katika tamthiliya ya *Morani* nadharia ya Simiotiki ni nadharia sahihi katika utafiti kama huu.

Nadharia ya Simiotiki kama inavyoelezwa na Barthes (1994) kuwa kuna misimbo mitano inayojenga nadharia hii. Misimbo hiyo ni kihemenitiki, kimuundo, kiishara,

kiutamaduni na kiseme. Msimbo wa Kihemenitiki unatokana na anuani ya kifasihi kama vile jina la kitabu, jina la shairi, jina la onyesho katika tamthiliya au jina la sura katika riwaya na hadithi. Wapo watunzi wa kazi za fasihi ambao hutunga kazi zao na kuzipa majina ambayo hufumbata maana ya kazi nzima. Msomaji anaposoma jina la kitabu hujikuta ameelewa maudhui mazima ya kitabu hicho. Kwa mfano, jina la tamthiliya ambayo tumeitafiti ni *Morani* ambalo ni jina linalomrejelea kijana wa jamii ya Kimaasai ambaye ni shupavu na hodari katika kuitetea jamii yake pamoja na mifugo dhidi ya adui. Kwa kuliona tu, jina hili la tamthiliya la *Morani*, mtunzi anaweza kuelewa maudhui yanayopatikana katika tamthiliya hiyo kuwa ni ya mapambano juu ya kitu fulani. Hii itamfanya asome kwa makini tamthiliya hii ili aweze kubaini kile ambacho kinapambaniwa.

Msimbo wa kimuundo wa nadharia ya Simiotiki ni ule unaoeleza namna mtunzi wa kazi ya fasihi anavyoweza kuunda visa na matukio katika kazi yake kwa njia ya kimsimbo (Nazarova, 1996). Anaweza kutumia mnyama au mdudu kuonyesha mdudu au mnyama huyo anafanya tukio fulani lakini tukio hilo kimsingi linarejelea tukio linaloweza kufanywa na binadamu. Mathalani, mtunzi wa kazi ya fasihi anaweza kutumia mnyama mbwa au paka kuonyesha namna anavyochukuwa chakula jikoni bila kupewa. Kimsingi, tukio hili linarejelea matukio yanayowafanywa na baadhi ya watu ambao wana tabia ya ubinafsi wa kujinufaisha wao wenyewe kutokana na rasilimali za umma. Matukio ya namna hii hujitokeza kwa kiasi kikubwa katika kazi za fasihi na kwa kutumia nadharia ya Simiotiki tunaweza kuelewa ni dhamira gani inayoelezewa kupitia msimbo huo wa kimatukio.

Msimbo mwingine ni wa kiutamaduni ambapo mtunzi wa kazi ya fasihi anaweza kutumia viashiria vya kiutamaduni kwa lengo la kuwasilisha dhamira katika kazi yake hiyo (Mark, 1995). Kwa mfano, kila jamii ina aina zake za vyakula, mavazi, ujenzi wa nyumba na shughuli za uzalishaji mali. Matumizi ya vitu hivi vya kiutamaduni huchangia sana katika kujenga dhamira kwa wasomaji na pale ambapo msomaji anaposoma kazi hiyo anaweza kuelewa dhamira iliyolengwa na mtunzi wa kazi ya fasihi.

Msimbo wa kiseme unatokana na elementi nasibishi ya kisemantiki ambapo neno fulani hutumiwa na mtumizi akiwa na maana inayokaribiana na maana ya msingi ya neno hilo. Mtunzi anaweza kutumia jina la mhusika sungura kumrejelea mhusika fulani katika kazi ya fasihi. Sungura ni mnyama ambaye ni mjanja anayeweza kufanya jambo lolote bila kushindwa kutokana na ujanja wake. Hivyo, mtunzi anavyomtumia mhusika huyu anakuwa anajenga taswira ya mtu ambaye ni mjanja na hivyo kwa kuchunguza ujanja huo tunaweza kuibua dhamira zilizolengwa kuifikia hadhira iliyolengwa.

Nadharia ya Simiotiki ina msimbo mwingine unaoitwa msimbo wa kiurejelezi au kiishara ambapo kunakuwa na matumiza ya lugha, matendo na matukio ya kiurejelezi yenye kulenga kuibua dhamira mbalimbali kwa hadhira iliyokusudiwa (Wamitila, 2002). Mtunzi wa kazi ya fasihi anaweza kumtumia mhusika fulani akionekana akipinga harakati za ukombozi wa jamii dhidi ya uhujumu uchumi. Tukio hili ni la kiurejelezi ambapo mhusika huyo anasawiriwa kuwa ni mtu asiyekuwa na elimu ya kutosha katika kupambana na maovu katika jamii na kwamba

elimu ni lazima itolewe kwa lengo la kuwaelimisha watu wa aina hiyo katika jamii. Nadharia ya Simiotiki imesaidia katika kuchambua data zilizohusiana na matumizi ya mbinu za kisanaa na dhamira katika tamthiliya ya *Morani*. Pia katika utafiti huu tumetumia nadharia ya Korasi katika kuchambua baadhi ya mbinu za kisanaa katika tamthiliya ya *Morani*.

2.5.2 Nadharia ya Korasi

Mutembei (2012) anapendekeza namna nyingine ya kuchambua kazi za fasihi kupitia mkabala wa Ki-korasi. Anasema, si jambo jema kushikilia kanuni na sheria za kufanya uhakiki wa kazi za fasihi unaosisitizwa na wanamapokeo bila kukubali mabadiliko yatokeayo katika sanaa ya fasihi. Hussein (1983) anaiona kazi ya sanaa kuwa ni mpya kila siku kwa sababu kazi ya sanaa ni kusawiri hali halisi ya maisha na maisha hubadilika kila siku. Hivyo, kusisitiza kanuni zilizowekwa na wanamapokeo katika uchambuzi wa kazi za fasihi ni kutozitendea haki kazi za fasihi.

Korasi ni neno lililokuwa likitumika katika kazi za fasihi tangu enzi za akina Plato na Aristotle. Katika kipindi hicho, Korasi ilijulikana kwa maana finyu hususani kwa kuhusishwa na mkarara katika kazi ya fasihi. Mkarara ni maneno, msitari au aya katika kazi ya fasihi inayorudiwa rudiwa ili kuleta mapigo ya kimuziki pamoja na kusisitiza jambo fulani. Mutembei (2012) alifanya utafiti juu ya korasi na kutoa mapendekezo kuwa, Korasi inaweza kutumika kama nadharia ya kuhakikia kazi za fasihi. Korasi inaweza kutazamwa kwa mapana zaidi ya mkarara kwani inaweza kujitokeza kama nyimbo, ngoma, jukwaa, wahusika, mchezo ndani ya mchezo, dhamira, jina la kitabu na sitiari kutaja kwa uchache. Msanii wa kazi ya fasihi anaweza akatumia kipengele kimojawapo kati ya vipengele vya korasi kujenga

dhamira mbalimbali katika kazi yake. Kwa mfano, katika kazi za tamthiliya huwa kunakuwa na matumizi ya nyimbo, nyimbo hizo huweza kurejelea dhamira au matukio tafautitafauti yanayojitokeza katika kazi husika. Ni msomaji makini pekee ndiye anayeweza kubaini kuwa matumizi ya wimbo fulani unasaidia kujenga dhamira fulani katika kazi anayoisoma. Emmanuel Mbogo ni mmojawapo kati ya watunzi wa tamthiliya atumiaye vipengele vya Kikorasi katika tamthiliya zake. Hivyo, nadharia hii imetumika katika kuchambua baadhi ya vipengele vya lengo mahususi la pili la tasinifu hii likihusisha vipengele kama wahusika na motifu.

2.6 Hitimisho

Katika sura hii tumewasilisha mapitio ya kazi tangulizi na mkabala wa kinadharia. Kazi tangulizi zinazohusiana na mada ya utafiti katika fani na maudhui zimepitiwa na kufanikiwa kubainisha mchango wa kazi hizo katika kufanikisha utafiti wetu. Tumeona watafiti kadhaa wakishughulikia tamthiliya za watunzi mbalimbali na hata zile za Emmanuel Mbogo. Matumizi ya mbinu za kisanaa katika tamthiliya ya *Morani* bado haijafanyiwa utafiti kama uliofanywa katika tasinifu hii. Nadharia za Simiotiki na Korasi pia zimewasilishwa katika sura hii na kuonyesha namna nadharia hizo zilivyotumika katika kuchambua data za utafiti huu.

SURA YA TATU

3.0 MBINU ZA UTAFITI

3.1 Utangulizi

Sura hii inahusu mbinu za kukusanya na kuchambua data za utafiti ili kuweza kufanikisha lengo kuu la utafiti huu. Mbinu za utafiti ni utaratibu unaoongoza namna utafiti unavyotakiwa kufanywa tangu katika kuteua sampuli ya utafiti, kukusanya, kupanga na kuchambua data za utafiti (Babbie, 1999). Ili kufanikisha kazi ya kukusanya data vipengele kuntu vimewasilishwa katika sura hii. Vipengele hivyo ni eneo la utafiti, usanifu wa utafiti, kundi lengwa, sampuli na usampulishaji, aina ya data zilizokusanywa, mbinu za kukusanyia data na mbinu za uchambuzi wa data.

3.2 Eneo la Utafiti

Eneo la utafiti ni mahali ambapo data za utafiti hukusanywa na wakati mwingine mahali zinapochambuliwa data za utafiti (Cresswell, 2009). Utafiti wa kisanyansi na kitaaluma kama huu lazima ufanywe katika eneo maalumu ambalo linaweza kutoa data sahihi kulingana na malengo ya utafiti. Eneo la utafiti lilikuwa ni mkoa wa Dar es Salaam katika manispaa ya Kinondoni mahali ambapo vinapatikana vyuo vikuu viwili ambavyo ni Chuo Kikuu cha Dar es Salaam na Chuo Kikuu Huria cha Tanzania. Utafiti huu ulikuwa ni wa maktabani na hivyo data za msingi na upili zilikusanywa kutoka katika maktaba hizo. Mtafiti aliamua kuteua maktaba hizi mbili kwa sababu zina machapisho ya kutosha ambayo yanahusiana na mada ya utafiti. Pia, maktaba hizi ziliteuliwa kwa sababu zipo karibu na hivyo kumfanya mtafiti asipoteze muda wakati anaposafiri kutoka maktaba moja kwenda nyingine. Hii

ilisaidia kupatikana kwa data sahihi za utafiti tena kwa muda mfupi.

3.3 Usanifu wa Utafiti

Usanifu wa utafiti ni mpango kazi unaoainisha njia na mikabala itakayozingatiwa katika kufanya utafiti hasa katika kukusanya, kuchambua na kuandika ripoti ya utafiti. Kothari (2008) anaeleza kuwa usanifu wa utafiti ramani inayochorwa kubainisha namna utafiti unaokusudiwa kufanywa ni wa aina gani, utatumia mbinu gani katika kukusanya na kuchambua data na matokeo ya utafiti yatawasilishwa kwa kutumia nyenzo gani. Usanifu wa utafiti huu ni uchunguzi kifani ambapo tamthiliya ya *Morani* iliyoandikwa na Emmanuel Mbogo imeteuliwa kwa ajili ya kufanyiwa utafiti. Uchunguzi kifani ni moja kati ya aina za usanifu wa utafiti ambapo eneo au kitu maalumu huteuliwa kwa ajili ya kufanyiwa uchunguzi wa kina kwa lengo la kupata matokeo fulani.

Uchunguzi kifani ni mbinu nzuri ambayo inamwezesha mtafiti kutumia muda wake vizuri kwa sababu tayari ameshateua kitu cha kukishughulikia na hivyo hana haja ya kuhangaika na mambo mengine yasiyohusiana na utafiti wake (Babbie, 1992). Pia, uchunguzi kifani humwezesha mtafiti kutumia rasilimali fedha kwa makini kutokana na kumakinikia jambo moja analolitafiti. Tamthiliya ya *Morani* ndiyo iliyotumika katika kukusanya data za msingi za utafiti huu na kuziwasilisha kwa njia ya madondoo katika sura ya nne. Uwasilishaji huo wa data umefuatiwa na uchambuzi wa kimaelezo yaliyoambatana na mawazo ya nadharia za Simiotiki na Korasi.

3.4 Kundi Lengwa

Kundi lengwa ni kipengele cha utafiti kinachorejelea wateule au watafitiwa wa utafiti

(Good, 1966). Kundi lengwa la utafiti huu lilikuwa ni tamthiliya ya *Morani* iliyotungwa na Emmanuel Mbogo. Tamthiliya hii iliteuliwa baada ya kubaini kuwa ni tamthiliya kongwe ambayo imekuwa ikisomwa kama kitabu cha kiada katika shule za sekondari katika nchi ya Tanzania kwa miaka mingi. *Morani* ni tamthiliya inayozungumzia maudhui juu ya uhujumu uchumi ambao kwa sasa umekuwa ni changamoto kubwa katika kuwanyima wananchi kupata maendeleo. Hata hivyo, hakuna utafiti wa mawanda mapana ambao umefanywa kwa lengo la kuchambua tamthiliya hii kama ilivyofanyika katika utafiti huu.

3.5 Sampuli na Usampulishaji

Sampuli ni sehemu inayoteuliwa kutoka katika kundi kubwa la watafitiwa kwa lengo la kutafitiwa ili kutoa data ambazo zitakuwa ni kiwakilishi cha kundi zima (Yin, 1994). Kwa kuwa si rahisi kwa mtafiti kufanya utafiti kwa kuwahusisha watafitiwa au kundi lote katika jamii, huteua sehemu ya watafitiwa hao ili iwe rahisi kuwatafiti kwa kuwahoji, kuwasaili na kusoma kama kinachotafitiwa ni kitabu. Sampuli ya utafiti huu ni tamthiliya ya *Morani* ambayo imeteuliwa kutoka katika tamthiliya zaidi ya 10 za mwandishi Emmanuel Mogo. Tamthiliya hii imeteuliwa baada ya kusoma kazi tangulizi na kubaini kuwa haijafanyiwa utafiti na hivyo kuhitajia kufanyika kwa utafiti huu ili kuziba pengo la maarifa na kukuza taaluma ya utafiti wa fasihi ya Kiswahili.

Usampulishaji ni kitendo cha kuteua sampuli kwa kutumia mbinu anuai za usampulishaji (Robson, 2007). Tamthiliya ya *Morani* ambayo ndiyo sampuli ya utafiti huu iliteuliwa kwa kutumia mbinu ya usampulishaji lengwa. Usampulishaji

lengwa ni mbinu ya kuteua sampuli kwa makusudi ambapo mtafiti anakuwa na uhakika kuwa sampuli hiyo ndiyo itakayomwezesha kupata data anazozihitaji. Tamthiliya ya *Morani* iliteuliwa kwa sababu mtafiti alifahamu kuwa tamthiliya hii itamwezesha kupata data alizokuwa akizihitaji. Usampulishaji Lengwa ni mbinu nzuri ya uteuzi wa sampuli kwa sababu humfanya mtafiti kutumia muda wake vizuri kwa kukiendea kile alichokiteua kwa ajili ya kukusanya data na kuachana na vingine ambavyo havihusiki katika utafiti wake (Cresswell, 2009).

3.6 Data Zilizokusanywa

Katika utafiti huu kumekusanywa data za aina mbili ambazo ni data za msingi na upili. Data hizi za aina mbili zimekusanywa kutokana na utegemezi uliopo baina ya data za msingi na upili kuwa ni wa kimkamilishano.

3.6.1 Data za Msingi

Data za msingi kama lilivyo jina lenyewe ni aina ya data ambazo zinakusanywa kwa mara ya kwanza kwa lengo ya utafiti kama huu na hazijawahi kukusanywa na mtafiti mwingine (Young, 1984). Data za msingi hukusanywa ili kuziba pengo la maarifa kama lilivyobainishwa katika sura ya kwanza sehemu ya tatizo la utafiti. Data za msingi za utafiti huu zilikusanywa kutoka katika tamthiliya ya *Morani* kwa kuzingatia malengo mahususi matatu ya utafiti huu.

3.6.2 Data za Upili

Data za upili ni data ambazo tayari zilikwishakukusanywa na watafiti watangulizi kwa lengo la kutimiza malengo ya utafiti wao (Babbie, 1999). Data hizi hukusanywa

kutoka katika machapisho na maandiko yaliyopo katika maktaba au mahali popote pale ambapo huhifadhiwa machapisho na maandiko kama nyumbani, ofisini, mkahawani na katika klabu za usomaji wa vitabu na magazeti. Data za upili za utafiti huu zilikusanywa kutoka katika machapisho na maandiko yaliyokuwa yanahusiana na mada ya utafiti katika maktaba za Chuo Kikuu Huria cha Tanzania na Chuo Kikuu cha Dar es Salaam.

3.7 Mbinu za Kukusanyia Data

Data za utafiti huu zilikusanywa kwa kutumia mbinu za usomaji makini na upitiaji wa nyaraka maktabani.

3.7.1 Mbinu ya Usomaji Makini

Usomaji makini ni mbinu ya kukusanya data za msingi kutoka katika maandishi ya kifasihi na hata yasiyokuwa ya kifasihi (Kothari, 2008). Mbinu hii imepewa jina la usomaji makini kwa sababu data za msingi zinapokusanywa humtaka mkusanyaji kuwa makini ili aweze kupata data stahiki za kuweza kujibu maswali ya utafiti wake. Mbinu hii imetumika kukusanya data katika tamthiliya ya *Morani* ambapo mtafiti aliisoma tamthiliya hiyo kwa kurudiarudia mara kadhaa mpaka pale alipoweza kupata data alizokuwa akizihitaji. Usomaji makini uliongozwa na malengo mahususi ambapo kila lengo lilipewa nafasi yake katika daftari maalumu la kukusanyia data. Msomaji alisoma tamthiliya hiyo mpaka alipojiridhisha kuwa amepata data za kutosha kujibu maswali ya utafiti wake.

3.7.2 Upitiaji wa Nyaraka

Upitiaji wa nyaraka ni mbinu ya kukusanya data za upili kwa mtafiti kusoma kazi

tangulizi zilizopo katika maktaba ambazo kwa namna moja au nyingine zinahusiana na mada ya utafiti (Robson, 2007). Mbinu hii hutumika kukusanya data ambazo zinasaidia kujazilishia data za msingi kwa lengo la kuzipa uhai zaidi. Upitiaji wa nyaraka huhusisha kusoma kazi tangulizi mbalimbali zilizopo katika maktaba kama vile tasinifu, majarida, makala, magazeti, vitabu, wavuti nantovuti. Upitiaji wa nyaraka ulifanyika katika maktaba za Chuo Kikuu Huria cha Tanzania na Chuo Kikuu cha Dar es Salaam.

3.8 Mbinu za Kuchambua Data

Baada ya data kukusanywa, kupangwa na kuwasilishwa ni sharti zichambuliwe ili ziweze kujibu maswali ya utafiti. Katika utafiti huu data zimechambuliwa kwa kutumia mkabala wa Kimaelezo.

3.8.1 Mkabala wa Kimaelezo

Mkabala wa kimaelezo ni mbinu ya kukusanya data kwa kuzitolea maelezo ambayo yanasaidia kujibu maswali ya utafiti (Kothari, 2008). Mkabala huu hutumika kuchambua data za kifasihi kama hizi za utafiti huu zilizokusanywa kutoka katika tamthiliya ya *Morani*. Baada ya data kukusanywa, kupangwa na kuwasilishwa kwa ajili ya uchambuzi, mtafiti ametolea maelezo madondoo yaliyowasilishwa kwa kuzingatia matakwa ya malengo mahususi. Kila lengo mahususi limepatiwa data na kuchambuliwa kwa njia ya maelezo ambayo yanakidhi vigezo vya kiutafiti. Mbinu hii ni nzuri kwa sababu uchambuzi unasomeka na kueleweka kwa uharaka kwa msomaji kuliko mbinu ya uchambuzi wa data ya kimahesabu. Katika uchambuzi wa

data pia tumetumia nadharia za Simiotiki na Korasi. Nadharia zilitumika kushadadia na kufafanua vizuri hoja zilizotokana na data za utafiti.

3.9 Usahihi wa Data

Data za utafiti huu ni sahihi na zinaaminika kwa sababu zimekusanywa na kuchambuliwa kwa kuzingatia mbinu halali za utafiti. Mbinu mbili za usomaji makini na upitiaji wa nyaraka ndizo zilizotumika katika kukusanya data. Mbinu hizi ni halali katika kukusanya data za utafiti wa maktabani kama huu wetu ambao umehusisha tamthiliya ya *Morani*.

3.10 Hitimisho

Sura hii imewasilisha mbinu na vipengele kadhaa vya kukusanya na kuchambua data za utafiti. Vipengele na mbinu zilizowasilishwa katika sura hii ni eneo la utafiti, usanifu wa utafiti, kundi lengwa, sampuli na usampulishaji. Vipengele vingine ni data zilizokusanywa; data za upili na msingi, mbinu za kuchambulia data; mkabala wa kimaelezo na usahihi wa data. Mbinu hizi zimetumika kukusanya data kwa kuzingatia malengo mahususi matatu ya utafiti huu hatua kwa hatua kwa hatua mpaka kufanikisha kuandikwa kwa tasinifu hii.

SURA YA NNE

4.0 UWASILISHAJI, UCHAMBUZI NA MJADALA WA DATA ZA UTAFITI

4.1 Utangulizi

Hii ni sura mama katika utafiti kwani ndiyo imefanya uwasilishaji, uchambuzi na mjadala wa data za utafiti. Mambo yote yaliyoelezwa katika sura zilizotangulia yalikuwa ni maandalizi tu ya kuwezesha kufanyika na kufanikiwa kwa sura hii. Data za utafiti zimechambuliwa kwa kutumia malengo mahususi ya utafiti ambayo yalikuwa ni kuchambua matumizi ya mbinu za kisanaa za tamathali za usemi katika tamthiliya ya *Morani*, kuelezea matumizi ya mbinu za kisanaa zisizo tamathali za usemi katika tamthiliya ya *Morani* na kubainisha dhamira zitokanazo na matumizi ya mbinu za kisanaa katika tamthiliya ya *Morani*. Tunaanza uwasilishaji, uchambuzi na mjadala wa data za utafiti huu na data zinalengwa katika lengo mahususi la kwanza la utafiti huu.

4.2 Mbinu za Kisanaa za Tamathali za Semi katika Morani

Tamthali za semi ni maneno au kauli fupi zilizosheheni lugha ya picha na ishara katika kuelezea na kufafanua dhamira katika kazi za fasihi simulizi na andishi (Wamitila, 2008). Tamathali za semi zimegawanyika katika makundi ya tamathali za mlinganisho na zisizo za kulinganisha. Tamathali za kulinganisha ni kama vile tashibiha, sitiari na tashhisi. Tamathali za usemi ambazo hazihusiani na ulinganishaji wa vitu ni kama mbalagha, kejeli, usambamba, takriri, kijembe, tafsida na kadhalika. Kwa kuwa si lengo la utafiti huu kutenga aina ya tamathali za semi, tumewasilisha,

kuchambua na kujadili tamathali za semi bila ya kujali kuwa ni tamathali ya ulinganishi au la.

4.2.1 Tashibiha

Matumizi ya lugha ya kitashibiha yanapewa nafasi kubwa na watunzi wa kazi za fasihi iwe simulizi au andishi (Wafula, 1999). Matumizi ya mbinu hii yamepewa nafasi hiyo kwa sababu ni tamathali ya semi ambayo hulinganisha vitu viwili au zaidi vyenye sifa tofauti kana kwamba ni vitu vinavyolingana. Tashibiha hutumia maneno ya kiulinganishi kama vile, ‘mfano wa,” “mithili ya,” “kama” na “anafanana na au kinafanana na.” Kwa kutumia maneno haya ya kiufananisho, vitu vinavyofanananishwa huonekana kuwa ni vitu vilivyo sawasawa kabisa na havina tofauti. Ni jambo la kawaida katika maisha kulinganisha vitu kwani ndipo msingi wa kupata dhamira unapoanzia. Kwa mfano, mwandishi wa kazi ya fasihi anaweza kuwa na tamathali ya usemi isemayo, “Mwanamboka ni mweusi kama mka.” Kutokana na tashibiha hii ambayo tunaambiwa kuwa weusi wa ngozi ya Mwanamboka ni sawa na weusi wa mkaa tunaweza kujenga dhamira kuwa kinachoelezwa hapa ni msisitizo kuwa Mwanamboka ni mtu mweusi asiyekuwa na mfano katika wanadamu wenzake hata anafananishwa na mkaa.

Mtunzi wa tamthiliya ya *Morani* naye ametumia tashibiha katika kuwasilisha dhamira kwa wasomaji wake. Katika matumizi hayo ya tashibiha, mtunzi anatoa msisitizo juu ya jambo ambalo anadhani ni muhimu kueleweka kwa wasomaji kwa namna ambayo inatoa uzito na uzingativu katika kuelewa. Kwa mfano:

JALIA: Umati! Umati wa watu sijapata kuona. Wake kwa waume. Vikongwe na watoto wa shule. Wafanyakazi na wakulima wamejaa tele! Naogopa!
MALONGO: Unaogopa!
MAPOTO: Unaogopa nini!
JALIA: Watu! Sijapata kuona umati wa watu kama huu. **Watu wengi kama sisimizi**. Barabara hazipitiki. Hewa angani imejaa nyimbo na mashairi ya kuwaponda mabepari, wahujumu uchumi na mabarakala. Wenye ngoma mbovu masikioni leo zitapasuliwa na midundo ya ngoma za wakonikoni. Wachawi wanatahayari. Nina hakika wameanza kufukiza ubani ili kuloga maandamano haya. Ni hatari (uk. 40).

Katika dondoo hili kuna matumizi ya tashibiha pale wingi wa wananchi waliojitokeza kushiriki katika maandamano wakilinganishwa na wingi wa sisimizi wanapokusanyika mahali pamoja. Tashibiha hiyo ni ile isemayo kuwa "watu wengi kama sisimizi." Umati wa watu wengi uliofurika katika maandamano ya kupiga vita uhujumu uchumi ni mkubwa sana kiasi cha kufananishwa na kundi la sisimizi. Sisizi ni wadudu wadogo wasio na kimo wala umbo kubwa na hivyo hata kuonekana kwao si kwa haraka kama ilivyo kwa wadudu wakubwa kidogo kama mbu, inzi, mende, nondo, vipepeo na wengineo. Jamii nyingine ya sisimizi ni mchwa na siafu lakini mchwa ni mkubwa kidogo kuliko sisimizi na siafu. Inapotokea sisimizi wakakusanyika kwa wingi mpaka inaonekana kuwa ni kundi kubwa bila shaka ni sisimizi wengi wasio na kifani. Mwandishi ametumia tashibiha hii kiishara kuashiria kuwa watu waliojitokeza katika maandamano hayo ni wengi mno jambo linaloashiria kuwa wananchi wengi wanachukizwa na vitendo vya uhujumu uchumi unaofanywa na viongozi wa umma (Sengo, 2009).

Pia matumizi ya mdudu sisimizi yametumiwa katika kujenga tashibiha hii kama kiwakilishi cha watu wanaoishi maisha ya chini ambao ndio wanaoumia kutokana na

uhujumu uchumi na rushwa unaofanywa na viongozi wa umma. Wananchi wa kawaida kama wakulima wadogo, wafugaji, wavuvi, wafinyanzi, wahunzi, mama na baba lishe na wafanyabiashara ndogondogo wanaofahamika kama wamachinga ndio wanaoumia kutokana na vitendo vya uhujumu uchumi vinavyofanywa na viongozi. Fedha zinazochukuliwa na viongozi kupitia rushwa na uhujumu uchumi ndiyo ambayo ingetumika katika kujenga shule, kununua vitabu, kujenga mabweni katika shule, kujenga zahanati, vituo vya afya, hospitali, kununua dawa na vifaa tiba na kuimarisha miundombinu ya usafirishaji, huduma za maji na umeme (Ryanga na Maina, 2012). Hivyo, fedha zinapokuwa zimechukuliwa na viongozi kupitia rushwa na ufisadi mwananchi wa kawaida anaishi maisha duni kwa sababu hawawezi kuwa na fedha za kwenda kupata huduma katika vituo vya afya na hospitali za binafsi kama ilivyo kwa viongozi ambao wanafedha nyingi walizowaibia wananchi. Wakati mtoto wa masikini anakaa chini badala ya kukalia dawati awapo shuleni, mtoto wa kiongozi anasoma katika shule nzuri za binafsi zenye mahitaji yote muhimu kwa elimu ya mwanafunzi. Haya ndio madhara ya uhujumu uchumi na rushwa kwa wananchi wa kawaida ndio maana wanaandamana upinga vitendo hivyo.

Mwandishi Emmanuel Mbogo anaendelea kutumia tashibiha katika tamthiliya ya *Morani* tena na kwa staili ambayo haijazoeleka. Tunasema kuwa ni kwa staili ambayo haijazoeleka kwa sababu imezoeleka kuona tashibiha ni ile inayotumia viunganishi au maneno ya kimlinganisho lakini hapa tunapata tashibiha kwa kutumia maneno ya ukanushi. Tazama mfano huu:

MLEMETA: Sina uhakika. (Anamshikashika.)
YUSUFU: **Yule Jalia si mwanamke, balaa**.

AISHA: **Jike-dume lile**. Haa! Maana hata alivyompigiza Mzee huyu mweleka wala sikumtambua. Ilikuwa spidi ya umeme. Hatari (uk.39)!

Katika dondoo hili mhusika Jalia ambaye ni mwanamke analinganishwa na mwanaume kutokana na ujasiri aliouonesha katika kumpiga mweleka mhusika mwingine aitwaye Nungu ambaye alikuwa ni mhujumu uchumi namba moja. Maneno kama, "yule Jalia si mwanamke, balaa," yanajenga tashibiha kwa wasomaji kiasi cha kuona kumbe Jalia anafananishwa na mwanaume kutokana na uwezo mkubwa alionao katika kupambana na wahalifu hasa wale wanaojihusisha na vitendo viovu vya rushwa, uhujumu uchumi na ufisadi.

Tamathali ya usemi aina ya tashibiha imetumika vizuri katika kutoa msisitizo wa dhamira ya uhujumu uchumi katika tamthiliya ya *Morani*. Mara nyingi jambo linapoelezwa kwa kutumia lugha ya kulinganisha hueleweka kwa haraka zaidi kwa wasomaji hasa pale vitu viwili vinavyolinganishwa wanavifahamu. Sasa tutazame matumizi ya tamathali ya semi aina ya mbalagha katika tamthiliya ya *Morani*.

4.2.2 Mbalagha

Mbalagha ni tamathali ya semi ambayo hutumiwa na watunzi wa kazi za fasihi kwa lengo la kueleza mambo kwa kutumia lugha ya kuongeza chumvi kwa kuelezea jambo hata nje ya uhalisia (Wamitila, 2008). Lengo la kutumia aina hii ya tamathali ni kutoa msisitizo na wakati mwingine kuonesha undani au ukubwa wa jambo lenyewe. Ikiwa jambo linaloelezewa ni njaa basi upo uwezekano kuelezwa kuwa kutokana na uhaba wa chakula ilifika mahali watu wakala vinyesi vyao. Katika hali

iliyozoeleka si jambo la kawaida kusikia mtu kala kinyesi chake kwani ni kitu chenye kutia kinyaa. Hata hivyo, katika ulimwengu wa fasihi jambo hili linawezekana na hutumiwa kwa makusudio maalumu.

Mtunzi wa tamthiliya ya *Morani* ametumia mbinu hii kwa lengo la kuonesha msisitizo juu ya masikitiko ya wananchi kutokana na hali ngumu ya maisha iliyosababishwa na uhujumu uchumi uliokuwa ukifanywa na viongozi na baadhi ya wafanyabiashara wakubwa. Masikitiko yao yalikuja pale kiongozi wao waliyemtegemea katika kupambana na uhujumi uchumi alipouwawa. Mtunzi anaeleza kuwa:

> MALONGO: (Kwa shaka.) Sijui… sijui kama hili dongo kweli lilididimia. Mimi naambiwa kuwa lilikuwa dege la shaba. Dege hili liliruka juu mawinguni, lakini macho yake makali yaliona kuwa lile dongo halikuwa dongo bali kitoweo. Lilitandaza mbawa zake likashuka. Lilipokaribia lile jabari lilinyoosha kucha za shaba na kulikwepua lile dongo. Dege lile likapaa juu; lilipenya mawinguni na kuingia mbingu ya saba. Dunia ilisimama, jua likajibanza mawinguni, mwezi ukageuka damu na nyota zikafinya. Watu walipiga yowe. Watu walilia: Uuuuiii! Uuuuii! Dongo! Dongo jamaa! … **Watu machozi yaliwatoka. Machozi yaliwatiririka watu. Mito ikafurika na mingine ikalowana kwa simanzi. Lakini haikusaidia kitu**. Vipofu wakaendelea kupapasa mitaa kwa matongotongo yao. Watoto waliendelea kuokota maboksi ya nyama zilizovunda. Na akina mama ntiliye wakafunga vibwebwe kuendelea kuchemsha makongoro. Hivyo ndivyo nilivyofahamu mimi. Habari ya kupasuka kwa jabari, kudidimia kwa dongo, mimi sijasikia (uk.01).

Dondoo hilo hapo juu lina matumizi ya mbalagha ambao unaonesha kuwa wananchi walilia sana baada ya kusikia kuwa kiongozi wao amefariki. Kipimo cha kilio walichokitoa ni wingi wa machozi yao yaliyotiririsha maji na kujaza mito. Katika uhalisia si kweli kuwa machozi ya watu yanaweza kujaza na kuifanya mito ifurike bali ni mvua tu tena mvua kubwa ndio yenye uwezo huo. Matumizi haya ya

mbalagha yamejengwa katika msimbo wa kiishara wenye kuonesha kuwa dongo linaloelezwa kuwa limedidimia ni kifo cha Waziri Mkuu wa Zamani wa Tanzania ndugu Edward Moringe Sokoine kilichotekea mwaka 1984 (Mutembei, 2012). Machozi yanayoelezwa hapa ni ishara ya inayoonesha kuwa wananchi walimpenda sana kiongozi huyo kwa sababu alikuwa akipigania haki zao kwa kukomesha uhujumu uchumi.

Matumizi mengine ya mbinu ya kisanaa ya kimbalagha yanajitokeza katika tamthiliya ya *Morani* kutoa msisitizo uleule wa kupiga vita uhujumu uchumu pamoja na wahujumu wenyewe. Mtunzi anasema:

> MZEE: Sikiliza, miti inaweza ikafanana rangi lakini ikawa kabila tofauti.
> MALONGO: Na utamu je? Mbona sawa? Mzee usije ukatupoteza.
> MZEE: Siuamini ulimi wako ambao haujaonja chakula kwa muda mrefu. **Katika hali kama hiyo hata sumu yaweza kuwa tamu**.
> MALONGO: Mbona husemi Mapoto? Ee?
> MAPOTO: Niseme nini (uk. 06)?

Dondoo hili limetumia mbinu ya mbalagha pale ambapo mtunzi anaposema kuwa sumu inaweza kuwa tamu. Hii ina maana kuwa wapo wahujumu uchumi ambao ni ndugu na wale ambao wamepewa dhamana ya kuhakikisha kuwa uhujumu uchumi unakomeshwa. Sasa itakuwaje katika kuwakamata watu hawa kwani itaonekana kuwa wamehusika katika kuwatafutia ndugu zao matatizo na serikali. Ndugu hao na wengine katika jamii hawatawaelewa wapingana na uhujumu uchumi iwapo watawatia hatiani ndugu zao. Hata hivyo, kazi ya kupambana na uhujumu uchumi lazima ifanywe hata kama ndugu anahusika katika uovu huo atajwe na kisha afikishwe katika vyombo vya sheria. Hapa mtunzi ametumia msimbo wa kiseme katika kufafanua ni kwa vipi sumu inaweza kuwa ni kitu kitamu (Cobley, 2001).

Kisemantiki, “sumu,” ni neno linalorejelea kitu chochote ambacho mwanadamu au mnyama akila au kikimpata katika mwili wake kwa namna moja au nyingine humdhuru na wakati mwingine hata kupoteza maisha. Hivyo, hakuna mtu hata mmoja ambaye anaweza kunywa sumu au kuacha akang’atwa na mdudu mwenye sumu kama nyoka kwa makusudi kwani anajua kuwa atadhurika.

Mbalagha wa sumu kuwa tamu pia unaweza kutazamwa kama ni msisitizo kuwa kazi ya kupambana na uhujumu uchumi na wahujumu uchumi ni ngumu na inaweza kumfanya mpiganaji kupoteza maisha yake. Mpiga vita uhujumu uchumi ni lazima aelewa kwamba kazi hiii ni ngumu na awe tayari kwa lolote lile litakalompata. Ni kazi hatari na ngumu kwa sababu inagusa maslahi ya watu ambao tayari walikwishazoea kupata vipato vikubwa kwa njia ambazo si halali. Katika dondoo lililopo hapo juu mtunzi anasema, “miti inaweza ikafanana rangi lakini ikawa kabila tofauti.” Kauli hii inasisitiza kuwa, wahujumu uchumi na mafisadi wapo wengi lakini si kila mhujumu uchumi unawez kumchukulia hatua kutokana na nafasi yake katika serikali na hata katika jamii. Kwa mfano, mhujumu uchumi anaweza kuwa ni kiongozi wa ngazi za juu serikalini ambapo namna ya kumtia hatiani inakuwa ni kazi ngumu. Hata hivyo, inapokuwa mhujumu uchumi ni mwananchi wa kawaida inakuwa ni jambo jepesi na rahisi kumkamata mhusika na kumpeleka katika vyombo vya sheria (Nicholous, 2011).

Mbinu ya kisanaa ya mbalagha iliyotumika katika tamthiliya ya *Morani* imeonesha kuwa kupambana uhujumu uchumi ni kazi ngumu inayohitaji umakini na moyo wa kujitolea na kutokuwa na uoga. Hata hivyo, imebainika kuwa inapokuwa ni kiongozi

wa ngazi ya juu serikalini ndiye mhusika mkuu katika uhujumu uchumi inakuwa ni vigumu kuchukuliwa hatua ikilinganishwa na wananchi wa kawaida (Sengo na Kiango, 2012). Jambo hili linahitaji utashi wa kisiasa hasa pale viongozi wa ngazi za juu watakopoona kingozi mwenzao anajihusisha na vitendo vya rushwa wanamchukulia hatua stahiki. Sasa tutazame mbinu nyingine ambayo ni matumizi ya takriri.

4.2.3 Takriri

Takriri ni aina ya tamathali ya semi inayotumika kwa kurudiwa rudiwa kwa silabi, neno, sentensi au aya katika kazi ya fasihi (Njogu na Chimerah, 1999). Mbinu hii hutumiwa na mtunzi kwa lengo la kusisitiza jambo ambalo anataka liingie kichwani kwa msomaji moja kwa moja bila ya kukwama kwama. Mtunzi hulazimika kutumia takriri kwa kuamini kuwa kama akieleza jambo lake kwa kutumia neno moja tu haitaeleweka vizuri kwa wasomaji wake. Matumizi ya mbinu hii yanajitokeza katika kazi nyingi za fasihi simulizi na fasihi andishi kutokana na umuhimu wake katika kufikisha dhamira kwa hadhira iliyolengwa na mtunzi. Mtunzi Emmanuel Mbogo katika *Morani* ametumia takriri mahala pengi na hata mwanzoni tu mwa tamthiliya yake hii kuna matumizi ya mbinu hii. Mfano mzuri wa takriri ni ule unaojitokeza katika uk.19 kuwa:

MLEMETA: Lakini mzee saa nane usiku sasa. Ingefaa turudi nyumbani tupumzike kwa muda mfupi halafu ndipo tuje tuendelee na kazi asubuhi.

DONGO: Nakwambia Mlemeta kama hii ni vita, na kama maadui zetu wanakesha usingezungumzia juu ya kuchoka, kupumzika na kusinzia. (Anapandisha sauti kidogo) Tutapumzikaje wakati miti yote imepukutika? Mlemeta tutapumzika wapi wakati telemkatukaze za wanyonge zimejaa kunguni na papasi? Huu ni wakati wa kunoa mashoka, siyo wakati wa kupumzika.

MLEMETA: Mzee … nadhani unajua unakotupeleka.

DONGO: (Anagonga meza kwa hasira) **NAJUA**!!!!!! **NAJUA**!!!!!! (Anasimama … anatembeatembea!!!!!! HASIRA!!!!!! Anamsogelea na kumsemea karibu kabisa na uso.) Mlemeta, wimbi linakwenda kasi na mwishowe litawazamisha ndumilakuwili wote kilindini. (Kimya) Mnaweza kutoka … (lakini wakikaribia mlangoni …) Mlemeta.

Dondoo hili linatoa msisitizo juu ya namna ya kuharakisha mapambano dhidi ya wahujumu uchumi kwa kupanga mipango madhubuti na kuitekeleza kwa makini. Mhusika Mlemeta anaoneka kuanza kukata tamaa ya kuwa hawataweza kufanikiwa katika mapambano na anaonesha kuwa amechoka anataka kupumzika. Dongo anamwambia hapana ninaelewa vizuri maelekezo ninayowapatia yatatuongoza katika kufanikisha mapambano dhidi ya wahujumu uchumi. Dongo anazungumza kwa msisitizo kabisa pale anaporudia neno, “najua” mara mbili ikiwa ni kutaka msimamo wake usiyumbishwe na uoga wa Mlemeta. Hapa mtunzi ametumia mbinu ya takriri kama nyenzo ya kuvunja mawazo ya uoga yanayoletwa na Mlemeta na hatimaye kusonga mbele katika harakati za kupambana na uhujumu uchumi. Wahujumu uchumi hawalali usiku kucha wakiwa katika jitihada za kuhakikisha wanafanikiwa kupora mali za umma, sasa iwaje wapambanaji nao walale mapema?

Hivyo ni lazima kwa wapambanaji wa vitendo vya uhujumu uchumi nao wakawa na mikakati ya kwenda sambamba na wahujumu uchumi ili kuwakomesha kwa kuwafikisha katika vyombo vya sheria na kutaifisha mali zao (Sengo, 1987). Takriri hii imetumiwa kwa kurejelea msimbo wa kiseme ambapo neno, “najua” kisemantiki ni neno lenye kuonesha kuwa na uhakika na jambo linalozungumzwa. Kwa muktadha huu ni uhakika alionao Dongo katika kuhakikisha kuwa mipango dhidi ya wahujumu uchumi inafanikiwa kutokana na umadhubuti wa mipango hiyo.

Matumizi mengine ya takriri yanajitokeza katika majibizano baina ya Nungu na Aisha mara baada ya Aisha kufukuzwa shule na sababu ikiwa ni ujauzito aliopewa na Nungu. Mtunzi anasema:

AISHA: Siku nyingi sijaenda shule mie. Mwezi. Walimu wamemletea barua Mzee. Wamenifuta. (Anataka kulia, anamkimbilia Nungu na kumkumbatia.) Utanisamehe Mpenzi Nungu.

NUNGU: (Anamsukuma) **Mpumbavu** mkubwa. Hutaki shule halafu unakuja kunililia mie? **Mpumbavu** mkubwa!

AISHA: **Mpumbavu**! **Mpumbavu** mimi! Mimi **mpumbavu**? Siku zote narudi saa nane usiku nyumbani baada ya heka heka za night club mimi na wewe. Ulitegemea nini? Ee?

NUNGU: (Kwa nguvu) Kelele! Sina hasara mimi. Si binti yangu, si chochote. (KIMYA) (uk.27).

Katika dondoo hili neno mpumbambavu limerudiwa mara tano kuonesha msisitizo kuwa mhusika anayeitwa Aisha ni mzembe kiasi cha kuruhusu kupata mimba na hali yeye ni mwanafunzi wa shule. Urudiwaji wa neno “mpumbavu,” kiasi cha mara tano ni ishara kuwa mwanaume anajitoa katika kumsababishia binti mdogo ujauzito hali binti huyo akiwa ni mwanafunzi. Suala la kujiuliza hapa ni kuwa, hivi kama mwanaume tena mtu maarufu mwenye utajiri kama Nungu amekosa nini cha kumwezesha kupata mwanamke mtu mzima wa kufanya naye mapenzi hata akamdanganya binti mdogo wa shule. Bila shaka anayetakiwa kuitwa mpumbavu hapa ni Nungu na si Aisha lakini mara nyingi hali huwa si hivyo kwani mwanamke ndiye huonekana kuwa ni mzembe pale mimba inapoingia bila kutarajiwa.

Matumizi ya neno “mpumbavu” yamejengwa kwa kutumia msimbo wa kiseme ambapo neno hili kisemantinki lina maana ya mtu anayefanya mambo bila ya kutumia akili kwa kuzingatia athari zitakazojitokeza kutokana na maamuzi aliyoyachukua (Mark, 1995). Neno hilo limetumiwa kutoa msisitizo juu ya dhamira

kuwa baadhi ya wanaume ambao ni matajiri hutumia utajiri wao kuwadanganya watoto wadogo na kufanya nao ngono zinazosababisha mimba za utotoni. Iweje mtu mzima kama Nungu tena tajiri amlaumu mtoto mdogo kama Aisha kuwa ni mpumbavu, bila shaka yeye Nungu ndiye mpumbavu na anapaswa kuchukuliwa hatua za kisheria ikiwemo kuhukumiwa kifungo cha miaka mingi jela.

Matumizi ya takriri neno, "mpumbavu" yametumiwa kama kejeli kwa baadhi ya watu ambao huwadanganya watoto wadogo wanaoweza kuwa sawa sawa na watoto wao na kushiriki nao katika ngono. Jambo hili linapaswa kukomeshwa kwa kila mtu kujua mipaka yake na kuheshimu nafasi ya mtoto wa kike kupata elimu na kuwa na maisha bora hapo baadae. Sasa tutazame matumizi ya mbinu ya lugha ya usambamba katika tamtiliya ya *Morani*.

4.2.4 Usambamba

Usambamba ni mbinu ya kisanaa ambapo mtunzi wa kazi ya fasihi hutumia lugha yenye kuonesha usambamba wa mambo ili kutoa msisitizo juu ya dhamira inayozungukiwa katika kazi ya kifasihi. Matumizi ya lugha ya usambamba hujenga aina fulani ya tamathali ya semi inayomvutia msomaji wa kazi ya fasihi kuisoma zaidi kazi hiyo. Hebu tuone mfano ufuatao:

JALIA: (Ameshika faili) sasa tumefika wapi?
MLEMETA: Mimi sina uhakika juu ya mpaka.
JALIA: Mpaka wa?
MLEMETA: Tazama: Kila kitu kina mpaka: **Mbingu mpaka wake ardhi**. **Moto mpaka wake maji**. **Giza mpaka wake mwanga**. **Mto mpaka wake bahari** (Anafikiri kidogo) Ila hii kampeni tu ndiyo haina mpaka … Ni hatari … Ndimi za moto zipendazo kuendelea kuivisha vyakula haziwezi kugombana na maji.

JALIA: (Mwanamke mwenye kiburi …) Sikiliza: Sisi kazi yetu ni kutayarisha orodha. Siyo habari ya mipaka.
MLEMETA: Lakini ni muhimu tujue mpaka wetu.
JALIA: Hivi mpaka wa kujilimbikizia mali ni upi? Ee? Ubarakala mpaka wake ni upi? Kama wale wanaokula mayai wana mpaka basi na sisi hatuna haja ya kuwa na mpaka.
YUSUFU: Sikiliza Jalia. Usishikilie jambo tu bila kujua matokeo yake ya baadaye. Hili suala tunalolishughulikia si dogo.
JALIA: Wala mimi sijasema kuwa dogo (uk.13).

Matumizi ya lugha inayoonesha usambamba yanajitokeza katika dondoo lililopo hapo juu kupitia maneno ya Mlemeta ya kwamba kila kitu kina mpaka wake na haifai kufanya jambo nje ya mipaka yake. Anasema kuwa, “mpaka wa mbingu ni ardhi, mpaka wa moto ni maji, mpaka wa giza ni nuru na mpaka wa mto ni bahari.” Maneno haya yamejengwa kwa usambamba unaotupatia tamathali nzuri kuisikia masikioni na hata kuiona kwa macho. Jambo la msingi linalooneshwa kupitia usambamba huo ni kuwa katika kampeni ya kupamabana na uhujumu uchumi ni lazima pawe na mipaka. Mipaka inayojengwa hapa ni kuwa ni nani na nani watazamwe kama wahujumu na nani na nani wasitazamwe kama wahujumu wa uchumi. Bila shaka, wanaolengwa kuwekewa mipaka ni watu maarufu ambao wamepata utajiri mkubwa kutokana na uhujumu uchumi akiwemo mhusika anayeitwa Nungunungu.

Mlemeta na Yusufu ndio ambao wanaonekana kusisitiza kuwa ipo haja ya kuweka mipaka katika kushughulikia wahujumu uchumi kwa sababu wahujumu wakubwa kama Nungunungu ni rafiki yao na wao wanapata chochote kutoka kwa mhujumu huyo na kwamba kama akikamatwa katika kampeni hiyo wao watakosa yale wanayoyapata kutoka kwa mhujumu huyo. Hata hivyo, Jalia anaonekana kutokukubaliana na suala la kuweka mipaka katika kupambana na wahujumu uchumi

kwa kuwa hakuna mipaka katika kujilimbikizia mali. Mawazo ya Jalia ni sahihi kwani pale mpaka wa kushughulikia uhujumu uchumi unapowekwa mwananchi wa kawaida ndiye anayepata taabu na kero nyingi za kodi zinamwangukia yeye. Kwa mfano, kama wahujumu uchumi wakubwa hawatashughulikiwa, mwananchi wa kawaida ndiye atakayebanwa katika kulipa kodi za kuendeshea serikali na wao mafisadi wakiendelea kuishi maisha mazuri yasiyo na kero.

Katika sehemu hii tumewasilisha, kuchambua na kujadili data zinazohusiana na lengo mahususi la kwanza la utafiti huu. Katika kutimiza lengo hili tumewasilisha na kujadili matumizi ya tamathali za semi za tashibiha, mbalagha, takriri na usambamba. Tamathali hizi zimejengwa kwa ustadi mzuri ambao unamwezesha msomaji kuzipata dhamira kama zilivyokusudiwa na mtunzi ziwafikie wasomaji wake. Katika sehemu inayofuata tumewasilisha data kuhusiana na lengo mahususi la pili la utafiti huu ambalo ni kubainisha matumizi ya mbinu za kisanaa zisizo tamathali za semi katika tamthiliya ya *Morani*.

4.3 Mbinu za Kisanaa Zisizo za Kitamathali katika Morani

Mbinu za kisanaa ambazo si za kitamathali ni zile zote ambazo hasihusiani na kauli fupi zenye kueleza mambo mengi kwa kuyafumbata kwa maneno machache. Mbinu hizi ni za jumla ambazo zinahusu matumizi ya methali, nyimbo, mtindo, muundo, wahusika, misemo, na mandhari. Matumizi ya mbinu hizi ni muhimu katika kuwasilisha dhamira kwa hadhira iliyolengwa na mtunzi wa kazi ya fasihi. Hata hivyo, katika tasinifu hii hatutazungumzia mbinu zote za kisanaa ambazo si za kitamathali bali baadhi tu kama ifuatavyo:

4.3.1 Matumizi ya Methali

Methali ni kauli zenye busara na hekima zitumiwazo na jamii kutoka kizazi hadi kizazi kwa lengo la kujenga maadili na kukuza ustaarabu katika maisha ya jamii. Methali ni kauli zenye pande mbili ambapo upande wa kwanza huwa ni swali na upande wa pili huwa ni jibu (Msokile, 1993). Kila jamii duniani ina methali zake kama ilivyo kwa jamii ya Waswahili. Methali ni kauli ambazo huibuka kila siku katika maisha ya jamii kutokana na shughuli za jamii za kila siku. Shughuli kama vile kilimo, ufugaji, uvuvi, ufinyanzi, ususi, biashara, kazi za ofisini, usafirishaji, viwandani, shuleni, kanisani, msikitini na hospitalini husaidia katika kuibuka kwa methali za Kiswahili. Uibukaji wa methali huwa haupangwi bali hujitokeza wenyewe wakati mwingine bila hata wanadamu kujua kama maneno au kauli iliyotolewa na mwenzao ni methali. Matumizi mapana ya kauli hiyo iliyoibuliwa na mwanajamii mmoja ndiyo baadaye hutambulika kuwa ni methali.

Matumzi ya mbinu ya kisanaa ya methali yanajitokeza katika tamthiliya ya *Morani* kuashiria kauli tuliyoitoa hapo awali kuwa methali ni kitu kinachotokea katika maisha ya kila siku. Mtunzi wa kazi ya fasihi ni mmoja kati ya wanajamii na hivyo katika utunzi wake methali hutokeza hata bila ya yeye kupanga kwamba ni lazima methali fulani iwepo ndani ya kazi yake. Methali kadhaa zinajitokeza katika *Morani* kama ifuatavyo:

> MALONGO: Mimi mashaka yangu ni kuwa labda hatutampata huyu shahidi.
> MZEE: **Penye nia pana njia**. **Na subira yavuta heri**.
> MAPOTO: Ila mimi wasiwasi wangu ni kuwa labda Dongo hana uwezo tena wa kuja kutusaidia … Nina shaka kama anakumbuka uswezi bado (uk.04).

Katika dondoo hili pamejitokeza methali mbili ambazo ni “penye nia pana njia na

subira yavuta heri.” Methali hizi kwa pamoja zimetumika katika kuwajenga wapambanaji wa uhujumu uchumi kuwa wavumilivu katika harakati zao za kupiga vita uhujumu uchumi. Kupambana na uhujumu uchumi ni kazi ngumu ambayo inamhitaji mpambanaji kutokata tamaa bali aamini kuwa siku moja atashinda. Mhusika Malongo anaonekana kuwa na wasiwasi kama Dongo anaweza kuwasaidia katika harakati za kumaliza uhujumu uchumi kwa sababu sasa yeye ni kiongozi mkubwa. Kiongozi kama ilivyo kwa Dongo tayari atakuwa ni rafiki mkubwa wa matajiri ambao baadhi yao ndio wahujumu uchumi. Sasa inawezekana vipi kwa mtu kumchukulia hatua kali za kisheria rafiki yake pale rafiki huyo anapofanya kosa kama la uhujumu uchumi? Hili ndilo swali linalomsumbua Malongo, lakini Mzee anatoa methali ya kwamba “penye nia pana njia na subira yavuta heri.”

Matumizi ya methali hizi yanawatia moyo akina Malongo na wenzake kufanya kazi kwa bidii ili siku moja waweze kufanikiwa kukomesha uhujumu uchumi katika jamii. Methali hizi zimejengwa kwa kutumia msimbo wa kiishara wa nadharia ya Simiotiki kwa lengo la kuwafanya wapambanaji kuwa na muda wa kutafakari kila maamuzi wanayofikia ili waweze kufanikiwa. Mtu anapokuwa na imani ya kwamba subira yavuta heri basi mtu huyo hutumia muda mwingi katika kufikiri namna bora ya kutatua tatizo au jambo lolote lililo mbele yake.

Methali za Kiswahili zinatumiwa kwa kiasi kikubwa na mtunzi Emmanuel Mbogo katika *Morani* ili kuijenga vizuri dhamira kuu ambayo ni uhujumu uchumi. Hebu tuone mfano ufuatao:

MLEMETA: Jina lako tayari liko kwenye orodha ya wahujumu uchumi mzee.
YUSUFU: Tumejaribu kila njia lakini haikuwezekana.

MLEMETA: Yule mtu kichwa maji hasa.
…
YUSUFU: Waswahili husema: **mwenzio akinyolewa, wewe tia maji!**
NUNGU: (Hasira) Una akili Yusufu! (Kimya) Nakuuliza; una akili?
YUSUFU: Mzee mimi nakutahadharisha tu.
MLEMETA: Hiyo haitasaidia kitu. Mzee hujui kuwa fimbo ya mbali haiui nyoka? Ukikimbilia nje utapambanaje nao?
NUNGU: (Kimya …) Ama kweli: Mfuga punda, fadhila hukujambia mashuzi. Maana aheri umsaidie mwenye donda, kuliko mwenye njaa. Tumeitoa nchi mbali, Ee! Tumejitolea maisha yetu sisi, Ee? Tumeiendeleza nchi sisi, Ee? Kwa jasho letu wenyewe tumechuma mali hii, Ee?! Leo … Leo … wanasema, wanatugeuka, wanatuita sisi wahujumu!! Tumehujumu nani? Wahujumu sisi (uk.23-24)??

"Mwenzako akinyolewa nawe tia maji," ni metahli iliyotumika kumtaka mhusika Nungu kujiweka tayari katika kukabiliana na namna ya kujitoa katika kundi la wahujumu uchumi. Tayari ameshataarifiwa kuwa yeye ni mmoja kati ya walioorodheshwa kuwa ni wahujumu uchumi. Katika harakati za kufanya maarifa ya kuepuka kufilisiwa mali zake na kufungwa jela, Nungu anaona kuwa njia bora ni yeye kukimbia nchi na kwenda kuishi ughaibuni. Hata hivyo, Mlemeta anatoa methali nyingine isemayo, "fimbo ya mbali haiui nyoka," akiwa na maana kuwa kama atakimbilia nje ndo atakuwa ameharibu mambo yote. Ni vema akabaki hapa nchini ili aweze kupambana na serikali na hatimaye arudishe heshima yake.

Methali hii imejengwa kwa kutumia msimbo wa kimatukio wa nadharia ya Simiotiki. Katika tukio la kuua nyoka ni sharti muuaji awe na fimbo ndefu ambayo itamwezesha kumpiga nyoka mpaka afe bila ya nyoka huyo kumdhuru kwa kumtemea sumu. Ikiwa fimbo ipo mbali haiwezi kumfikia nyoka na mpigaji akilazimisha kusogeza fimbo yake ambayo ni fupi anaweza kung'atwa au kutemewa sumu na nyoka huyo (Eco, 1976).

4.3.2 Matumizi ya Wimbo

Wimbo ni moja katika bahari za ushairi wa Kiswahili ambao unaelezwa na Shaaban Robert kuwa wimbo ni shairi dogo (Njogu na Chimerah, 1999). Wimbo ukiwa mmoja na nyimbo zikiwa mbili na kuendelea, kuna nyimbo za harusi, misiba, sherehe za halaiki, kuapishwa viongozi, nyimbo za siasa, nyimbo za taifa, nyimbo za kuhamasisha utendaji kazi na nyimbo za dini. Nyimbo hutumiwa kwa malengo mbalimbali katika jamii lakini hasa ni kuburudisha, kuelimisha na kufunza maadili mema katika jamii. Nyimbo ni kipera katika utanzu wa ushairi ambacho kinaonesha kuwa na uhusiano wa karibu sana na maisha ya wanadamu ya kila siku. Matukio mengi yanayofanyika katika jamii huambatana na nyimbo na pale nyimbo zinapotumika shughuli husika huwa nzuri na ya kupendeza.

Kwa kulitambua hili hata watunzi wa kazi za fasihi andishi kama Emmanuel Mbogo katika *Morani* ametumia nyimbo ili kuifanya kazi yake inoge na ifikishe ujumbe vizuri kwa hadhira yake. Matumizi ya wimbo katika *Morani* yanajitokeza kama ifuatavyo:

JALIA:	Lazima ugeuze macho na midomo kama makongoro kweli. La sivyo wimbo hauwezi kupendeza.
MALONGO:	Wewe subiri tu: (Anaanzisha wimbo) Maji yakipwa huingia Wimbi la wafanyakazi Kuanzisha mapambano Dhidi ya ubarakala na Uhujumu uchumi … (x2)
KIITIKIO	
MAKONGORO:	Waziri amehujumu, aa sawa hiyo?
WAIMBAJI:	Haata, Hiyo si sawa Waziri acha vituko!
MAKONGORO:	Wana madola Uswizi, aa, sawa hiyo?
WAIMBAJI:	Haata, Hiyo si sawa jamani acha vituko!
MAKONGORO:	Unga hauonekani, aa, sawa hiyo?
WAIMBAJI:	Haata, Hiyo si sawa jamani wacha vituko!

MAKONGORO: Meneja kapewa rushwa, aa, sawa hiyo?
WAIMBAJI: Haata, Hiyo si sawa Meneja, wacha vituko!
MAKONGORO: Meneja kwa wasichana, aa, sawa hiyo?
WAIMBAJI: Haata, hiyo hiyo sawa meneja acha vituko!

(Polepole giza linaingia jukwaani).

Wimbo huu umejitokeza mwishoni kabisa mwa tamthiliya ya *Morani* si kwa bahati mbaya bali kwa makusudi mazima ya kumtaka msomaji aipate vizuri dhamira ya uhujumu uchumi. Mutembei (2012) anaeleza kuwa kitendo cha Emmanuel Mbogo kuuweka wimbo huu mwishoni mwa tamthiliya yake kumefumbata dhamira kuu inayozungukiwa katika tamthiliya ya *Morani* kwa kutumia mbinu ya korasi. Matukio yote yaliyotokea na kuelezewa katika tamthiliya hii yanajitokeza katika wimbo na mtu akiusoma wimbo huu anaweza kupata ufahamu wa mambo ya msingi yanayojitokeza katika *Morani*.

Kupitia wimbo huu kunatajwa baadhi ya wahujumu uchumi miongoni mwao wakiwa ni mawaziri na mameneja. Ikiwa hali ndio hii ni vigumu kupambana na uhujumu uchumi kwa sababu wahusika wakuu ndio waliopewa jukumu la kuhakikisha kuwa hakuna mtu yeyote anayejihusisha na vitendo vya kuhujumu uchumi. Mtunzi anatumia kejeli pale anaposema, “aa, waziri acha vituko, aa, meneja acha vituko,” kuwasema viongozi wanaojihusisha na kuhujumu uchumi wa nchi. Waziri au meneja na mtumishi mwenye mshahara na marupurupu makubwa ambayo yanamwezesha kuwa na maisha mazuri lakini bado kiongozi kama huyo anafanya vitendo vya kuhujumu uchumi ili aendelee kupata kipato kikubwa zaidi (Sengo, 1973). Ama kwa hakika hiki ni kituko kama anavyokiita mwandishi Emmanuel Mbogo.

Katika wimbo huu pia kunatajwa madhara ya uhujumu uchumi kwa wananchi wa maisha ya chini hasa pale bidhaa muhimu zinapokosekana madukani. Bidhaa ya unga wa sembe hutumiwa na watu wengi katika kupika ugali na wengine uji na kufanya sehemu ya chakula chao kikuu. Bidhaa kama hii inapokosekana sokoni husababisha watu wa chini kupata adha kubwa ya chakula kwa sababu hawana uwezo wa kununua mchele ambao huuzwa aghali kuliko unga wa sembe. Kiongozi aliyechaguliwa na wananchi kwa ajili ya kuwatumikia wananchi wake lakini yeye anajihusisha na vitendo vya uhujumu uchumi ambavyo vinamfanya mwananchi wa kawaida ateseke, si kiongozi huyo bali ni kituko. Kiongozi anatakiwa kuwa msitari wa mbele katika kuhakikisha kuwa wananchi wake wanapata unafuu katika gharama za maisha na si yeye kuwa ni sehemu ya kuongeza ugumu wa maisha kwa watu wake tena waliompigia kura ya ndiyo na kuwa kiongozi (Nyerere, 1967). Viongozi wa aina hii si tu wanatakiwa kunyimwa uongozi lakini pia wanatakiwa kufikishwa katika vyombo vya sheria ili wahukumiwe kwa makosa ya uhujumu uchumi na kuwasababishia wananchi maisha magumu. Wimbo huu umejengwa kwa kutumia nadharia ya Korasi ambapo, kutokana na wimbo huu tumeweza kupata dhamira ya uhujumu uchumi ikiwa inajitokeza kwa mapana na marefu (Mutembei, 2012).

4.3.3 Wahusika wa Kikorasi

Wahusika ni watu, vitu, wanyama, miti, wadudu na mawe ambao hutumiwa na watunzi wa kazi za fasihi kwa ajili ya kuwasilisha ujumbe kwa hadhira iliyokusudiwa. Wahusika hawa ndio wanaotenda matendo mbalimbali ambayo ndani mwake mna dhamira zilizolengwa kwa hadhira fulani iliyoteuliwa na mwandishi. Mutembei (2012) anaeleza kuwa mhusika wa kikorasi ni yule ambaye athari ya

matendo, maneno, tabia na kauli zake zinakuwa na mchango katika kujenga dhamira za kazi ya fasihi kwa namna moja au nyingine anatoa hatma ya maudhui katika kazi hiyo. Kwa mfano, mhusika Karama katika riwaya ya *Kusadikika* ya Shaaban Robert ni mhusika wa kikorasi ambapo kupitia kauli na matendo yake anatoa mustakabali mzima wa dhamira katika riwaya hii. Mbinu hii ya kutumia mhusika kama korasi inajitokeza katika tamthiliya ya *Morani* kama ifuatavyo:

> MAPOTO: Tena risala itowe mwito kwa **Morani** Wote. **Morani** waungane na umma. Waungane ili kuendeleza safari. Kuendeleza safari ya kuitafuta nguzo ya Uswezi. (Anaandika)
> JALIA: Na nguzo ya Uswezi itapatikana. Itapatikana wanyonge waisimike, wailinde na kuanza kuijenga nyumba (uk.43).

Maelezo yanayotolewa na mhusika Mapoto yanataja aina ya mhusika ambaye tunamwita kuwa ni mhusika wa Kikorasi. Anasema, "tena risala itowe mwito kwa Morani Wote. Morani waungane na umma." Hawa Morani wanaotajwa hapa wanarejelewa wapiganaji wote wa vita ya uhujumu uchumi. Wahusika kama vile akina Jalia, Mapoto, Makongoro na Dongo ndio wanaorejelewa kupitia mhusika Morani. Matendo yote yanayofanywa na wahusika hao tangu mwanzo wa tanthiliya mpaka mwisho yanaonesha kweli wao ni "Morani." Morani ni kijana wa Kimaasai ambaye ni shupavu, hodari na mwenye ujuzi wa hali ya juu katika kupambana na maadui. "Morani" ni kijana ambaye anao uwezo wa kupambana na simba na wanyama wengine ambao ni hatari kwa maisha ya wanadamu mpaka akamuua mnyama huyo. Hivyo, kwa kumtaja mhusika "Morani" hapa ambaye anajumuisha wahusika wote wenye kupinga uhujumu uchumi ni korasi inayozungukia ukweli kwamba vita dhidi ya uhujumu uchumi ni kali na isiyoweza kushindwa kwa urahisi. Lakini "Morani," akidhamiria kupata ushindi katika jambo lolote lile mara nyingi

hufanikiwa. Hivyo, vita dhidi ya uhujumu uchumi itafanikiwa ikiwa Morani wote wataungana na kuwa kitu kimoja.

Mtunzi amemtumia mhusika “Morani” kama korasi katika kuonesha kuwa katika vita dhidi ya uhujumu uchumi jamii inakosa umoja na mshikamano na badala yake wengine wanawatetea wahujumu wasichukuliwe hatua za kisheria zinazostahiki. Hata hivyo, mhusika “Morani” ni mtu mwenye msimamo asiyekubali kuyumbishwa katika maamuzi. Hili linathibitishwa na maamuzi ya Dongo na kupambana na wahujumu uchumi hata kufikia akauwawa akiwa katika vita hivyo. Kama wapiganaji wote wangemuunga mkono kwa kuwa morani wa kweli kama yeye na akina Jalia, vita dhidi ya uhujumu uchumi ingeshinda.

Mhusika wa kikorasi anajitokeza pia katika tamthiliya ya *Morani* kupitia maelezo aliyoyatoa Nungu na hali yake ilipobadilika ghafla tunaelezwa kuwa bundi alilia kwa sauti yake kisha akaondoka. Hebu tuone mfano ufuatao katika *Morani*:

> NUNGU: …wanasema, wanatugeuka, wanatuita sisi wahujumu!! Tumemhujumu nani?! Wahujumu sisi?? Tumemhujumu nani?! Hata hao wanaojitia kimbelembele na kutamba, bila sisi … (Tunasikia sauti ya **Bundi**, Nungu anakimbia na kufungua dirisha. Nguvu zinamwishia ghafla) Loo! Amekuja!! Nilidhani haji! (**Bundi** anaendelea kulia kwa sekunde chache kisha anaondoka. Kimya!! Lakini Nungu bado yupo palepale.) (Mlemeta na Yusufu wamekuwa wanastaajabia maajabu haya na hasa Yusufu, wanamuona akiwa katika hali ya kupumbaa, anapagawa, anatetemeka na kutikisika mwili mzima; anarudi na kukaa pale kitini.) (uk.24).

Mhusika “Bundi,” anayetajwa katika dondoo hapo juu ni mhusika wa kikorasi kutokana na ukweli kuwa mlio wa sauti yake huashiria jambo baya la huzuni kama vile msiba au janga ambalo lina athari kwa maisha ya mwanadamu. Mlio huu wa

bundi umetoa ishara juu ya namna mambo yanavyokwenda katika tamthiliya ya *Morani* ambapo mwishoni mwa tamthiliya tunashuhudia kifo cha Dongo mpambanaji mashuhuri katika vita dhidi ya ufisadi. Sambamba na hilo, pia mhusika "Bundi" ametumika kikorasi katika kutoa mlio wa ishara ya kuangamia kwa wahujumu uchumi wakubwa kama Nungunungu alipumbaa hata asijuwe uamuzi wa kuchukua baada ya kuambiwa kuwa naye ni mmoja kati ya waliorodheshwa katika orodha ya wahujumu uchumi. Kwa vyovyote vile, hili ni janga kubwa kwa Nungunungu kwani saa na wakati wowote mali zake zitataifishwa na yeye kuishia jela. Hivyo, mhusika "Bundi," anajenga dhamira pana ya uhujumu uchumi katika tamthiliya ya *Morani* tangu mwanzo mpaka mwisho wa tamthiliya hii.

4.3.4 Motifu ya Namba

Motifu ni mbinu ya kisanaa inayotumiwa na watunzi wa kazi za fasihi katika kuwasilishia dhamira na ujumbe kwa hadhira iliyokusudiwa kutokana na marudiorudio ya dhana fulani katika kazi hiyo. Kwa mfano, inawezekana mtunzi akawa na wahusika katika kazi yake ambao sifa yao kuu ni kusafiri kila siku kutoka mahali fulani kwenda mahali pengine. Safari za wahusika katika kazi za fasihi hazifanywi hivi hivi tu bali huwa na sababu maalumu ambayo kifasihi husaidia katika kujenga dhamira kwa wasomaji (Wamitila, 2008). Kwa mfano, mhusika anaweza kusafiri kutoka katika nchi yake kwenda nchi nyingine kwa ajili ya kujifunza jambo fulani lenye manufaa kwake binafsi na kwa jamii nzima. Kutokana na maana hii ya motifu tunaweza kuwa na aina kadhaa za motifu ambazo ni motifu ya bibi kizee, mama wa kambo, motifu ya msako, motifu ya safari na motifu ya namba (Senkoro, 1997).

Mathalani, Motifu ya namba 7 inajitokeza kwa wingi katika tamthiliya ya *Morani* ikiwa na dhima maalumu ya kufikisha ujumbe kwa hadhira iliyokusudiwa. Senkoro (1997) anaeleza kuwa katika jamii ya Waswahili ni jambo la kawaida kuona kila jambo likisemwa kuwa ilipofika siku ya 7 ilikuwa hivi au vile, maharusi walipewa siku 7 za kupumzika mara baada ya kufunga ndoa, tanga lilianuliwa baada ya siku 7 na watu wakatawanyika, rais alitoa siku 7 kwa mamlaka ya mapato kuhakikisha kuwa inakusanya kodi kwa wafanyabiashara waliokwepa kulipa na ilipofika siku ya 7 mtoto aliyepotea alipatikana. Mfano wa motifu hii katika *Morani* ni kama ifuatavyo:

> MALONGO: Mimi nimechoka! (Kimya). Mzee nimechoka
> MZEE: Basi tupumzike kidogo chini ya mti huu. (Wote wanakaa isipokuwa Malongo ambaye anakwenda kuokota matunda yaliyodondoka chini … anawagawia wenzake … wanakula … Mzee anasimama, anakitazama kilima kilichopo mbali … kinatoa moshi …) Ulikuwa udongo … udongo uliokauka, kisha udongo ukaloa kwa mvua za radi. Radi zikachimbua na kufinyanga ule udongo wa mfinyanzi … Lile jitu lenye kichwa chenye busara, lile jitu lenye vidole kumi, kucha nyeupe, lilikokota udongo ule wa mfinyanzi. Likaufinyanga. Siku ya kwanza, na ya pili. Siku ya tatu dongo likawa tayari. Siku ya nne dongo lile likawekwa mikono na miguu. Siku ya tano vidole, ya sita macho, ya saba dongo likawa tayari. Lile jitu likalilaza lile dongo juu ya jabari ili likauke. Kisha lile jitu likapotelea hewani na kurudi tena siku ya kumi na saba: Patupu! (Kimya kidogo.) Kumbe tazama: Jabari lilikuwa limepasuka na dongo limedidimia, limedidimia dongo ndani ya udongo. Na hayo ndio maajabu ya dunia (uk.01).

Dondoo hili lina matumizi ya motifu ya namba 7 ambapo tunaelezwa juu ya tukio la kuumbwa kwa dongo ambalo liliundwa kwa siku takribani 6 na ilipofika siku ya 7 lilikamilika. Baadaye yule muumbaji wa jitu hilo aliondoka na kupotelea hewani hata ilipofika siku ya 17 alikarudi tena. Motifu hii ya namba 7 imetumiwa hapa kujenga dhamira ya namna ya kupambana na uhujumu uchumi kwa kwa kuweka mipango

thabiti. Uhujumu uchumi ni jambo baya kwa sababu linasababisha watu wachache kuwa matajiri wakubwa na wengi wa wanajamii kuwa maskini wa kutupwa. Hivyo, kupambana dhidi ya uhujumu uchumi kunawahitaji wahusika kukaa chini na kutafakari kwa makini juu ya mipango na mikakati itakayosaidia wanajamii kukomesha uhujumu uchumi. Kutafakari jambo kwa siku 7 ni muda mzuri wa kutosha kumfanya mfikiriaji kupata maarifa mapya ya kuandaa mipango na mikakati maridhawa itakayosaidia kukomesha vitendo vya uhujumu uchumi katika jamii. Mipango itakayopangwa kwa ajili ya kupambana na uhujumu uchumi ni lazima iwe na muda maalumu kwani bila muda maalumu kupangwa ni vigumu kwa mipango hiyo kutekelezwa kwa makini.

Katika dondoo hapo juu kunaelezwa kuwa muumbaji alirudi siku ya 17 kuja kutazama maendeleo ya kile alichokiumba. Siku aliyorudi ina namba saba pia jambo linaloonesha kujirudiarudia kwa nambari hiyo na kujenga motifu ya namba 7. Namba 7 na 17 ni namba ambazo zinagawanyika kwa zenyewe na kwa 1 peke yake. Hii ni sawa na kusema kuwa ni namba tasa. Katika kujiuliza swali la kwamba hivi ni kwa nini inatumika namba hii katika miktadha ya aina tofautitofauti tumegunduwa kuwa namba 7 hutumiwa kwa sababu maalumu. Kwanza ni namba tasa ambayo inagawanyika kwa yenyewe na kwa 1 tu. Hivyo, siku 6 zinatosha kulifanya jambo likatengamaa na siku ya 7 ikawa ni siku ya kulihitimisha jambo hilo. Hivyo, ni dhahiri kuwa upo uwezekano wa jambo kukamilika ndani ya siku 7 na kupatikana hitimisho lililokuwa linakusudiwa. Viongozi wa serikali wamekuwa wakiitumia sana motifu ya namba 7 pale wanapotaka ripoti juu ya jambo fulani ambalo ni muhimu kutoka kwa mtumishi wa serikali aliyepewa wadhifa au mamlaka katika taasisi ya

umma na hata katika taasisi binafsi. Na mara nyingi baada ya siku 7 ripoti hutolewa na maamuzi huchukuliwa.

Sehemu hii imewasilisha, kuchambua na kujadili data za utafiti zinazohusiana na lengo mahususi la utafiti ambalo lililenga kubainisha mbinu za kisanaa zisizo za kitamathali katika tamthiliya ya *Morani*. Mbinu hizo za kisanaa zilizowasilishwa katika sehemu hii ni matumizi ya methali, matumizi ya wimbo, wahusika wa kikorasi na motifu ya nambari 7. Mbinu hizi za kisanaa zimesaidia katika kuibua dhamira katika tamthiliya ya *Morani* ambapo msomaji huburudika lakini wakati anaburudika pia hupata dhamira zilizokusudiwa na mwandishi. Sehemu inayofuata inawasilisha, kuchambua na kujadili data zinazohusiana na lengo mahususi la tatu la utafiti huu ambalo ni kuchambua dhamira katika riwaya ya *Morani*.

4.4 Dhamira katika Tamthiliya ya Morani

Tamtiliya ya *Morani* ni moja kati ya tamthiliya za mwanzo mwanzo za mwandishi Emmanuel Mbogo iliyosheheni dhamira mbalimbali zenye umuhimu mkubwa katika kuihakiki jamii ya Watanzania. Dhamira kuu katika tamthiliya hii ni uhujumu uchumi ambao ulikuwa unafanywa na viongozi wa serikali na kujinufaisha wao wenyewe na kuwaacha wananchi wakiishi maisha ya umaskini. Dhamira ya uhujumu uchumi inajitokeza kwa namna mbalimbali katika tamthiliya *ya Morani*. Uwasilishaji wa dhamira ya uhujumu uchumi katika *Morani* ni kama ifuatavyo:

4.4.1 Uongozi na Uhujumu Uchumi

Dhamira ya uongozi na uhujumu uchumi ni jambo ambalo limekuwa likizungumzwa na serikali za awamu zote zilizotawala katika nchi ya Tanzania. Viongozi wa umma

wanaonekana kushiriki katika vitendo vya uhujumu uchumi kwa njia za rushwa na ufisadi kiasi cha kuwa na utajiri mkubwa wa kutisha (Nyerere, 1977). Serikali imekuwa ikifanya jitihada kubwa katika kuhakikisha kuwa vitendo vya uhujumu uchumi vinakoma na fedha za umma zinatumika katika miradi ya kuwaletea wananchi maisha bora na kuwapatia maisha bora. Miongoni mwa jitihada zilizofanywa na serikali ni kuanzisha Taasisi ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa (TAKUKURU). Taasisi hii imekuwepo kwa miaka mingi lakini bado vitendo vya rushwa, ufisadi na uhujumu uchumi vinaendelea kufanywa na baadhi ya viongozi na pia baadhi ya wananchi. Emmanuel Mbogo katika tamthiliya ya *Morani* anasema:

> DONGO: … Ebu nileteee faili la siri.
> HADIKWA: La nani Mzee?
> DONGO: La Nungunungu. (Anapewa faili) Unamwonaje Mlemeta, Hadikwa?
> HADIKWA: Kwa vipi mzee?
> DONDO: Kwa vyovyote vile (Kimya kidogo) kikazi kwa mfano.
> HADIKWA: Nadhani ni kiongozi hodari. Ana bidii ya kazi.
> DONGO: Kweli? (Kimya kidogo) Mlemeta anafanana na tai asiyeweza kutua ardhini kwani miguu yake imeota majipu yaliyoiviana: Inabidi aendelee kuelea angani kama kishada … Hadi lini? Sijui.
> HADIKWA: Chai yako inapoa mzee.
> DONGO: (Anakunywa ile chai …) Nungunungu na Mlemeta ni kama kupe na mkia wa ng'ombe. Unafahamu hiyo Hadikwa?
> HADIKWA: Sina uhakika mzee.
> DONGO: (Anacheka kidogo) Uhakika utaupata wapi? Unazungumza kama hakimu. Mahakimu wetu hawahukumu mtu hadi wapate ushahidi wa uhakika. Watu kama Nungunungu ni … (uk.09).

Dondoo hili linajengwa kwa kutumia lugha ya mafumbo ambapo Mlemeta kama kiongozi wa umma anashirikiana na wafanyabiashara wakubwa katika viyendo vya uhujumu uchumi. Mlemeta anatajwa kuwa ni mtu ambaye amezungukwa na majipu yaliyoiva mwili mzima na kwamba yapo tayari kutumbuliwa. Mtunzi anasema, "Mlemeta anafanana na tai asiyeweza kutua ardhini kwani miguu yake imeota

majipu yaliyoiviana," kauli ya kimafumbo inayoonesha kuwa Mlemeta ni mla rushwa asiye na kifani. Katika hali ya kawaida, jipu ambalo limeiva lipo tayari kukamuliwa saa yoyote na likishakamuliwa hupona. Hata hivyo, majipu ya Mlemeta yametokea katika miguu kiasi cha kumfanya ashindwe kutembea bali aende juu juu kama ndege aina ya tai. Hii ni lugha ya kifasihi inayoashiria kuwa Mlemeta ni kiongozi aliyekubuhu katika vitendo vya uhujumu uchumi na kwamba hawezi kukwepa kukamatwa na kushitakiwa kwa vitendo hivyo ambavyo ni viovu (Mosoti, 1993).

Kimsingi, Jipu ni aina ya upele unaompata binadamu na baadhi ya wanyama ambapo ndani ya jipu huwa mnakuwa na usaha ambao ukishaiva unatakiwa ukamuliwe uishe wote na damu itoke ndipo mwenye jipu apone. Hapa kuna matumizi ya lugha yaliyojengwa katika msimbo wa kimatukio wenye kuhusisha tukio la mtu kukamuliwa jipu na kufukuzwa katika nafasi ya uongozi na kuchukuliwa hatua za kisheria. Dawa ya kiongozi mla rushwa ni kumfukuza kazi na kumchukulia hatua za kisheria ili ahukumiwe kulingana na makosa aliyoyafanya.

Katika jamii ya Watanzania kumekuwepo na vitendo vingi vya viongozi kushiriki katika vitendo vya rushwa na ufisadi kiasi cha rais wa Tanzania Mheshimiwa Dkt. John Pombe Joseph Magufuli kufananisha hali hiyo na jipu. Wakati akihutubia bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa mara ya kwanza alisema, "Serikali yetu imejaa majipu ambayo ni watumishi wala rushwa na mafisadi na mimi nimejipa kazi ya kuwa mtumbua majipu. Ili jipu lipone ni lazima likamuliwe usaha wote utoke na kufuatiwa na damu, hakuna dawa nyingine zaidi ya hii." Kauli ya mheshimiwa

rais inaonesha kufanana na ile inayopatikana katika tamthiliya ya *Morani* iliyotungwa na Emmanuel Mbogo. Hatua za makusudi zinapaswa kuchukuliwa ili kuhakikisha kuwa uhujumu uchumi, rushwa na ufisadi vinatokomezwa haraka iwezekanavyo ili kuwafanya wananchi wa kawaida waweze kuishi maisha mazuri.

Kimsingi suala la kupambana na wahujumu uchumi linahitaji mashirikiano baina ya viongozi wote katika serikali. Ikiwa baadhi ya viongozi wanawatetea wahujumu uchumi vita dhidi yake haiwezi kufanikiwa kama ilivyokusudiwa (Sengo, 2009). Katika tamthiliya ya *Morani* tunafahamishwa kuwa baadhi ya viongozi walikuwa na ari na moyo wa kupambana na wahujumu uchumi lakini wengine walikuwa ni kikwazo. Kwa mfano:

> DONGO: Mlemeta lazima uelewe kuwa ushahidi ni sanaa ya walaji dhidi ya wanyonge, lakini mantiki ni sanaa ya wanyonge dhidi ya walaji (Akisoma faili) Kwa mfano: Nungunungu, kwa nini hamkumwandika?
>
> MLEMETA: Mzee hii kampeni nia yake kuvuruga au kujenga? Kwa sababu lazima tuwe waangalifu, la sivyo tutajikuta tumetumbukiza mikono yetu katika mafuta yanayotokota. Tutachubua ngozi mzee.
>
> DONGO: Mlemeta katika mapambano haya msumemo utakata pande zote. Aidha tufanye kazi ama tuache. Lakini hatuwezi kuchanganya kazi na unafiki. Kama tumekubaliana kwa pamoja kuwa wahujumu wote wakamatwe, basi watakamatwa … (anafungua faili la Nungunungu) Mlemeta unataka nikutajie madhambi ya ndugu yako (uk.12).

Majibizano ya viongozi hawa wawili yanaonesha kuwa hawakubaliani katika harakati za kupambana na uhujumu uchumi. Hali hii ni njia mojawapo inayoonesha kuwa mapambano dhidi ya uhujumu uchumi ni kitu kigumu na hakiwezi kufanikiwa bila viongozi wote kuwa wamoja na hata wanajamii pia kuungana kwa umoja wao. Majibizano haya yanaonesha kuwa baadhi ya viongozi katika serikali wanashiriki katika vitendo vya uhujumu uchumi na kwa hivyo wahujumu wakichukuliwa hatua

za kisheria viongozi hao watabainika au hawatanufaika tena kwani mhujumu hatakuwepo tena uraiani. Mfano hai wa hiki kinachoelezwa katika *Morani* upo katika jamii ambapo rais wa Tanzania amewasimamisha kazi viongozi mbalimbali kutokana na kuhusika katika vitendo vya rushwa, ufisadi na uhujumu uchumi.

Uhujumu uchumi ni kitu ambacho kinawafanya wanaojihusisha nacho kuwa matajiri na kuishi maisha mazuri (Wafula, 1999). Hivyo, si jambo jepesi kumtaka mtu ambaye tayari anapata utajiri kwa kutumia nija za uhujumu uchumi aache kwani kwa kufanya hivyo atakuwa anapoteza fedha zinazomfanya kuwa tajiri na kuishi maisha mazuri. Hebu tuone mfano ufuatao:

JALIA: Ninyi ndio mnaotuvurugia nchi. Mbona husemi chochote kuhusu karafuu na tanzanaiti mnayovusha nje kwa magendo ili kuchuma madola? Mbona husemi lolote kuhusu madola yenu mliyoyalundika ughaibuni. Hata ufunike mavi kwa bakuli haitasaidia kitu!

NUNGU: Huo nao ni utoto na ujinga. Mna ushahidi au mnazua tu maneno na kuwapaka watu matope.

JALIA: Hakuna haja ya kumpaka mtu matope kama mtu huyo kachuchumaa msalani anajinyea mavi yake mwenyewe. Vitu vimepanda bei, chumvi, mchele, unga, sukari, sabuni kila kitu. Ninyi tu mnayelalia magodoro ya manoti ndiyo mnazimudu hizo bei. Makabwela na watoto wao wakale wapi (uk.30).

Maelezo ya Jalia yanaonesha utajiri mkubwa walionao wahujumu uchumi na umaskini wa wananchi wa kawaida unaowafanya washindwe kununua mahitaji muhimu katika maisha yao ya kila siku. Wahujumu uchumi wana fedha nyingi mpaka nyingine wamekwenda kuzihifadhi katika mabenki ya nchi nyingine sembuse ya kiasi cha fedha kilichohifadhiwa katika benki za ndani. Kupambana na watu wa aina hii ni kazi ngumu mno kama wapambanaji hawataungana na kuwa kitu kimoja. Tunasema hivi kwa sababu hakuna binadamu ambaye yupo tayari kuacha kufanya

kitu ambacho kinampatia fedha kirahisi, lazima atafanya kila mbinu ili kuhakikisha anaendelea kupata fedha kama kawaida.

4.4.2 Maisha Magumu

Maisha magumu ni hali ya watu kushindwa kumudu gharama za maisha yao ya kila siku kutokana na kipato duni, sera mbaya za serikali, uhujumu uchumi, rushwa na ufisadi na kukosekana na bidhaa muhimu kama mafuta ya kuendeshea mitambo na vyombo vya usafiri (Msokile, 1993). Ukosefu wa vitu hivi huwafanya wananchi kushindwa kupata mahitaji ya msingi kama chakula, malazi na mavazi na kuwafanya kuwa na hali ngumu kimaisha. Katika mazingira ya leo tunapozungumza juu ya maisha magumu tunakwenda mbali zaidi na kuhusisha mtu anapoumwa na kushindwa kupata matibabu kwa sababu hana fedha, kukosa maji safi na salama ya kunywa, kushindwa kulipa karo ya shule kwa watoto na kukosa miundombinu ya uhakika ya usafirishaji. Mwandishi wa *Morani* Emmanuel Mbogo anasawiri hali ya maisha magumu katika tamthiliya yake pale anaposema:

JALIA: (Kama mtu anayehutubia.) Tuandike risala kwa lugha itakayoamsha chuki dhidi ya ubeberu na ukoloni mamboleo. Risala yenye mishale ya sumu. Sumu itakayounguza maini na mapafu ya wahujumu uchumi, mabepari, mabepari uchwara, vibaraka na vibarakala popote walipo.

MAPOTO: Tena risala hii ieleze jinsi maisha yalivyo magumu kwa watu wa hali ya chini. Ieleze jinsi maduka yalivyojaa vitu vya bei za kutisha. Makabwela na watoto wao wakiendelea kuandamwa na utapiamlo. (Anaandika).

JALIA: Tena risala hii ieleze jinsi nchi hii ilivyo tajiri: ardhi tele, maji, maziwa, mito, mamilioni ya ng'ombe, mbuzi, kondoo, samaki … Na kwamba kusingizia hali ya hewa na opeki ni uzandiki-dhambi nyekundu pyu isiyofutika wala kusameheka. (Anaandika).

MAPOTO: Tena risala hii ifichue siri kwamba fedha zetu kidogo za kigeni hazitumiki kwa kuendeleza kilimo. Badala yake madola

> yanatumika kununua vitu vya anasa ili kuwanufaisha wachache. (Anaandika) (uk.42).

Dondoo hili linathibitisha kuwa wananchi wanaishi maisha duni kutokana na athari za uhujumu uchumi unaofanywa na viongozi wakishirikiana na baadhi ya wafanyabiashara. Vitendo hivyo vya uhujumu uchumi vinafanya vitu muhimu kwa matumizi ya binadamu ya kila siku kupanda bei na wao kushindwa kumudu bei hizo na hatimaye kuwa na maisha magumu. Mwandishi anaeleza kuwa athari za maisha hayo magumu ni wananchi kupata utapiamlo ugonjwa unaosababishwa na ukosefu wa lishe bora. Mwananchi mwenye utapiamlo hawezi kufanya kazi za uzalishaji kwa ufanisi kwa sababu afya yake imezorota. Mwandishi anaeleza kuwa fedha za kigeni za umma zinatumika katika kununua vitu vya anasa kwa ajili ya viongozi badala ya kutumika katika kuendeleza na kukuza kilimo. Kilimo ndicho kinachotoa ajira kwa wananchi wengi wa Tanzania pamoja na kuhakikisha usalama wa chakula nchini. Inakuwaje fedha za kigeni za umma zitumike kununua vitu vya anasa kwa ajili ya viongozi wachache ambao hawafiki hata asilimia moja ya wananchi wote? Huu ni ufisadi, rushwa na uhujumu uchumi ambao unapaswa kukomeshwa na utokomee kabisa.

Katika dondoo hili pia kunaelezwa kuwa Tanzania ni nchi yenye utajiri mkubwa wa rasilimali mbalimbali ambazo zinaweza kuwaondoa wananchi katika umaskini. Haiingii akilini nchi yenye rasilimali nyingi kama Tanzania kuwa katika orodha ya nchi maskini duniani. Utumiaji mbaya wa rasilimali hizi ndio unaofanya wananchi kuwa na maisha magumu na hata kupata utapiamlo. Rasilimali za taifa zinatumiwa kuwanufaisha watu wachache kupitia mikataba isiyo na tija waliyotiliana saini na

wawekezaji katika sekta za madini, ardhi, utalii, hoteli na utoaji wa huduma mbalimbali kwa jamii (Muysoka, 1996). Mwandishi anaeleza kuwa vitendo vya uhujumu uchumi vitaendelea kuifanya Tanzania kuwa maskini mpaka pale tu vitendo hivi vitakapokomeshwa. Mkomeshaji wa vitendo hivi kwa kiasi kikubwa ni mwananchi kwani yeye ndiye mwenye uwezo wa kumuweka au kumuondoa kiongozi fulani katika madaraka. Mwandishi wa *Morani* ameliona suala hili ndio maana katika maelezo yake anasisitiza kuwa ni lazima risala ieleze hivi na vile ili kuamsha ari ya wananchi katika kudai haki zao na kutetea mustakabali wa nchi yao. Wananchi wakishaelewa wajibu wao katika kuwawajibisha viongozi bila shaka watawaondoa katika nafasi za uongozi wale ambao ni wahujumu uchumi na wala rushwa na kuchagua vingozi makini wenye nia ya dhati ya kuwaletea wananchi maendeleo ya kweli.

4.4.3 Matabaka

Matabaka ni hali ya kuwepo kwa makundi katika jamii kulingana na uwezo wa kipato kutoka kundi moja na jingine. Hali hii inafanya kuwepo kwa tabaka la juu na tabaka la chini ambapo tabaka la juu ni la matajiri na tabaka la chini ni la maskini (Msokile, 1993). Uwepo wa matabaka haya hutegemeana ambapo utajiri wa tabaka la juu unatokana na umaskini wa tabaka la chini. Hii ni sawa na kusema kuwa kuna unyonyaji baina ya matabaka ambapo tabaka la chini ndilo ambalo hunyonywa na tabaka la juu (Sengo, 1987). Suala la matabaka katika jamii ni la kihistoria kwani limekuwepo tangu pale mwanadamu alipoanza kuishi katika dunia kwa mashirikiano na wanadamu wenzake. Kwa mfano, Adamu na Hawa ndio wanadamu wa kwanza kuumbwa na kuishi katika ulimwengu kwa mara ya kwanza. Walikuwa ni watu

wawili tu lakini utabaka wa kijinsia ulikuwepo ambapo Adamu ndiye aliyekuwa kiongozi wa Hawa na hivyo yeye akapewa daraja ya juu na Hawa akapewa daraja ya pili.

Tatizo linalojitokeza hivi sasa ni kuwa tofauti za kipato katika matabaka zinazidi kukuwa kila siku kiasi cha kuwafanya wale wa tabaka la juu kuwa matajiri zaidi na wale wa tabaka la chini kuwa maskini zaidi. Ukweli wa mawazo haya unapatikana katika tamthiliya ya *Morani* kama anavyosema mwandishi:

> MALONGO: Kwanza tazama. Juhudi yote tuliyofanya katika ile safari imekuwa kazi bure. Safari ilikuwa ndefu; usiku, mchana, mvua, miba, njaa, kiu … lakini matokeo yake ni haya. Akina Nungu wanatumbua, akina yakhe wanazidi kutumbukia. (Anafikiri)
> MAPOTO: Nadhani kuna mahali tulikosea.
> MALONGO: Nakwambia Mapoto, paka hawezi kupigana na chui.
> MAPOTO: Siyo kila siku … Wakati mwingine anaweza. Vipi, kwa mfano ufunguo mdogo unaweza kufungua lango kubwa? Hii ni siri ambayo yatubidi tuichimbue (uk.35).

Malezo ya Malongo yanaonesha kukata tamaa ya kwamba wamefanya jitihada kubwa katika kupambana na uhujumu uchumi lakini bado hawajafanikiwa. Hawajafanikiwa kwa sababu tofauti kati ya tabaka la juu na la chini inaendelea kukuwa kila siku. Anasema, “akina Nungu wanaendelea kutumbua na akina yakhe wanaendelea kutumbukia,” ambapo akina Nungu ndio tabaka la juu na akina yakhe ni tabaka la chini. Malongo anaonesha nia ya dhati ya kupambana na wahujumu uchumi ii kupunguza utabaka ni wananchi wa chini kuamua kupambana na wahujumu uchumi. Hata hivyo, Malongo anaona kuwa watu wa tabaka la chini hawana uwezo wa kupambana na watu wa tabaka la juu. Anasema, “nakwambia Mapoto paka hawezi kupigana na chui,” ikiwa ni kauli yenye kuonesha kuwa paka ni tabaka la chini na chui ni tabaka la juu.

Hapa mtunzi ametumia msimbo wa kiishara ambapo chui ni mnyama wa mwituni ambaye ni mkali sana katika mawindo yake na paka ni mnyama wa nyumbani mwenye upole ukimlinganisha na chui. Mapoto anaonekana kutokukubaliana na mawazo ya Malongo kwa kuwa anaamini kwamba upo uwezekano wa wananchi wa tabaka la chini kuwashinda watu wa tabaka la juu ikiwa watu hao wataungana pamoja. Katika uhalisia, watu wa tabaka la chini ni wengi kuliko wale wa tabaka la juu na hivyo ni rahisi sana kuwashinda kama wakiungana na kuwa kitu kimoja. Kama ufunguo ambao ni mdogo unaweza kufungua mlango mkubwa ndipo watu wakaweza kuingia ndani ya nyumba sasa iweje wananchi walio wengi washindwe na wachache? Waswahili wana methali isemayo, “umoja ni nguvu na utengano ni udhifu,” na hivyo wananchi wanatakiwa kuungana katika kupigania haki zao.

4.4.4 Haki na Usawa

Haki na usawa ni dhamira ambayo inatokeza katika kazi nyingi za fasihi zikiwemo tamthiliya za Emmanuel Mbogo na hasa hii ya *Morani*. Haki ni msamiati unaotumika kurejelea stahiki anayotakiwa kuipata mtu kwa mujibu wa sheria na taratibu zinazoelekeza namna haki hiyo inavyotakiwa kutolewa kwa walengwa. Kwa mfano, kila mwananchi ana haki ya kuishi maisha yake anavyotaka ilimradi asivunje katiba ya nchi na sheria nyingine zitakazo na katiba hiyo (Sengo, 2009). Inapotokea mtu amefanyiwa vitendo vyovyote vyenye kuhatarisha haki yake ya kuishi atakuwa ananyimwa haki yake ya msingi ya kuishi kwa amani. Ili haki iweze kutendeka ni lazima kuwepo na usawa katika jamii. Haki inaweza kupatikana pale tu panapokuwa na usawa katika jamii. Watu wote bila ya kujali vipato vyao wanatakiwa kutazamwa kuwa ni sawa kwa sababu wote ni binadamu.

Usawa katika jamii unaonekana kutokuwepo kutokana na mambo mbalimbali lakini kubwa likiwa ni uhujumu uchumi ambao unawafanya baadhi ya watu kuwa na fedha nyingi za kununua majaji na mahakimu. Katika tamthiliya ya Morani mwandishi anaeleza:

> MALONGO: (Kalewa kidogo) Haya! Tazama juzi. Nimekwenda mahakamani. Kichekesho. (Anakunywa) Basi unajua? Yule jaji alifungua mbuku wake mweusi wa sheria akasoma: (Anasimama, anaigiza.) Kamati na mahakama imechunguza na kuona kuwa hakuna ushahidi wowote wa kuthibitisha kuwa Ndugu Nungunungu amekuwa anajihusisha na biashara ya haramu za kuhujumu uchumi wa nchi. Mahakama hii inaridhika bila mashaka yoyote kuwa ushahidi uliotolewa dhidi ya Nungunungu ni majungu matupu yenye nia ya kumpaka matope. Hivyo mahakama imeamua kumwachilia ndugu Nungunungu huru! (Okasha na hasa Yusufu na Aisha wanapasuka kwa vicheko.) (uk.35).

Dondoo hili linaonesha kuwa licha ya kuwa Nungunungu ni mhujumu uchumi namba moja lakini anaachiliwa huru na mahakama. Usawa na haki katika jamii hauwezi kupatikana katika mazingira kama haya. Ilikuwa ni haki ya Nungunungu kuhukumiwa kifungo cha miaka mingi jela kutokana na makosa ya uhujumu uchumi ambayo amekuwa akiyafanya lakini cha ajabu anachiliwa huru kwa madai kwamba hana kosa na ni watu tu ambao ndio wanataka kumpaka matope.

4.5 Hitimisho

Tamthiliya ya *Morani* imepambika kwa mbinu kuntu za kisanaa zikiwemo za matumizi ya lugha ya tamathali za usemi na tamathali zisizo za usemi ambazo kwa pamoja zimeweza kuwasilisha dhamira kwa hadhira. Mbinu za kitamathali zilizowasilishwa katika sura hii ni tashibiha, mbalagha, takriri na usambamba na mbinu zisizo za kitamathali ni matumizi ya methali, matumizi ya nyimbo, wahusika

wa kikorasi na motifu ya namba. Mbinu hizi za kisanaa zimesaidia kuibua dhamira za uongozi na uhujumu uchumi, maisha magumu, matabaka na haki na usawa.

SURA YA TANO

5.0 HITIMISHO, MUHTASRI NA MAPENDEKEZO

5.1 Utangulizi

Sura hii itatoa hitimisho, muhtasari na mapendekezo ya utafiti mzima kwa lengo la kuukamilisha.

5.2 Muhtasari

Utafiti huu ulikuwa na malengo mahususi matatu ambayo katika muhtasari huu kila lengo litaelezwa kwa ufupi. Malengo hayo yalikuwa ni kuchambua matumizi ya mbinu za kisanaa za tamathali za usemi katika tamthiliya ya *Morani*, kuelezea matumizi ya mbinu za kisanaa zisizo tamathali za usemi katika tamthiliya ya *Morani* na kubainisha dhamira zitokanazo na matumizi ya mbinu za kisanaa katika tamthiliya ya *Morani*.

5.2.1 Mbinu za Tamathali za Usemi

Lengo mahususi la kwanza lililenga kuchambua mbinu za kisanaa za tamathali za usemi katika tamthiliya ya *Morani* ambapo mbinu nne zimewasilishwa na kuchambuliwa. Mbinu hizo ni tashibiha, mbalagha, takriri na usambamba. Katika muhtasari huu tutaeleza kwa ufupi juu ya tashibiha, mbalagha na usambamba. Matokeo ya utafiti yanaonesha kuwa katika tamthiliya ya *Morani* kuna matumizi ya tashibiha hususani pale wananchi walipokuwa wakiandamana kupinga vitendo vya uhujumu uchumi katika nchi yao. Moja kati ya tashibiha tuliyoiwasilisha katika uchambuzi wa data ni “watu wengi kama sisimizi” ikiwa ni ulinganisho wa idadi ya watu waliojitokeza katika maandano hayo ya kuwapinga mabepari na wahujumu

uchumi. Mshabaha huu unaashiria kuwa wanajamii hawapendi kabisa vitendo vya uhujumu uchumi kwa sababu vinachangia katika kurudisha nyuma maendeleo ndio maana walijitokeza kwa wingi mithili ya sisimizi katika maandamano.

Matumizi ya mbinu ya mbalagha nayo yanaonesha namna wanajamii walivyochukizwa na kitendo cha kuuawa kwa mpambanaji wa vita dhidi ya uhujumu uchumi. Dongo alikuwa ni kiongozi namba moja katika kupambana na wahujumu uchumi lakini aliuawa na kifo chake kilisababisha simanzi kubwa katika jamii. Tulidondoa sehemu hii katika sura ya nne na kuifanyia uchambuzi, “watu machozi yaliwatoka. Machozi yaliwatiririka watu. Mito ikafurika na mingine ikalowa kwa simanzi. Lakini haikusaidia kitu.” Katika uhalisia hakuna machozi yanayoweza kujaza mto hata yawe mengi kiasi gani. Lakini huu ni uthibitisho kwamba wananchi walimpenda sana Dongo kiongozi makini katika mapambano dhidi ya uhujumu uchumi na kifo chake kiliwahuzunisha mno.

Mbinu ya usambamba nayo tumeiwasilisha katika uchambuzi wa data na matokeo ya utafiti yanathibitisha kuwa usambamba umetumika kuonyesha kuwa mapambano dhidi ya uhujumu uchumi si kitu chepesi hata kidogo. Sehemu tuliyoidondoa katika uchambuzi wa data ilisema, “mpaka wa mbingu ni ardhi, mpaka wa moto ni maji, mpaka wa giza ni nuru na mpaka wa mto ni bahari.” Huu ni usambamba uliotumika kurejelea kuwa mapambano dhidi ya uhujumu uchumi yana mipaka yake na hivyo wapo baadhi ya watu hata kama ni wahujumu uchumi hawawezi kuchukuliwa hatua stahiki. Watu hawa ni viongozi na watu maarufu wakiwakilishwa na akina Mlemeta na Nungunungu. Hata hivyo, sheria za kupambana na uhujumu uchumi na rushwa

pamoja na ufisadi ni lazima zifanye kazi bila ubaguzi ili kukomesha vitendo hivyo viovu na adui wa maendeleo.

5.2.2 Mbinu za Kisanaa Zisizo za Kitamathali

Lengo mahususi la pili la utafiti huu lililenga kuelezea matumizi ya mbinu za kisanaa ambazo si za tamarhali za usemi katika tamthiliya ya *Morani*. Nia ya lengo hili ilikuwa ni kubainisha mbinu mbalimbali za kisanaa katika *Morani* ambapo tulifanikiwa kuelezea mbinu za matumizi ya methali, matumizi wa wimbo, wahusika wa kikorasi na motifu. Kwa muhtasari tumeelezea matumizi ya methali na wahusika wa kikorasi. Matumizi ya methali yamejitokeza katika *Morani* ambapo methali kama vile, “penye nia pana njia na subira yavuta heri,” zimewasilishwa na kuchambuliwa katika sura ya nne. Methali hizi zimetumika kwa lengo la kuwahamasisha wapambanaji dhidi ya uhujumu uchumi kuwa na matumaini kwamba siku moja watafanikiwa. Haitakiwi kukata tamaa ya mapambano licha ya kuwepo kwa changamoto zinazokwamisha kufanikiwa kwa mapambano hayo.

Katika lengo mahususi la pili pia tumebainisha mbinu ya matumizi ya wahusika wa kikorasi katika tamthiliya ya *Morani*. Mhusika wa kikorasi ni yule ambaye anatumika kuwarejelea watu wengi kwa mara moja huku akibeba dhamira muhumu kwa jamii. Tulidondoa sehemu ifuatayo ili kuelezea namna mhusika wa kikorasi anavyojitokeza katika Morani, “tena risala itowe mwito kwa Morani wote. Morani waungane na umma.” Morani ni mhusika aliyetumiwa kikorasi kurejelea wapambanaji dhidi ya uhujumu uchumi kuwa ni watu hodari na wasiokata tamaa katika mapambano.

5.2.3 Dhamira katika Morani

Lengo mahususi la tatu la utafiti huu lilihusu kubainisha dhamira zitokanazo na matumizi ya mbinu za kisanaa katika *Morani*. Dhamira zilizobainishwa katika lengo hili ni uongozi na uhujumu uchumi, ugumu wa maisha, matabaka na haki na usawa. Matokeo ya utafiti yamebainisha kuwa viongozi wanashirikiana na wahujumu uchumi katika kuhujumu rasilimali za taifa na kulifanya taifa kuendelea kuwa masikini. Imezoeleka katika jamii kuona viongozi wa kisiasa wakipatiwa fedha na watu ambao wanasadikika kuwa ni wahujumu uchumi katika kipindi cha kampeni za kuomba uongozi. Baada ya viongozi hao kuchaguliwa na kuingia madarakani hushindwa kuwachukulia wahujumu uchumi hatua stahiki. Hali hii huwafanya wahujumu uchumi kuwa na nguvu hata za kuifanya mahakama ishindwe kutoa haki na badala yake kuwaachia wahujumu uchumi bila kuwaadhibu.

5.3 Hitimisho

Matumizi ya mbinu za kisanaa katika *Morani* yamefanikiwa kuipamba na kuiwasilisha vizuri dhamira kuu katika tamthiliya hiyo ambayo ni uhujumu uchumi. Mbinu za kisanaa za tamathali za usemi na zile ambazo si tamathali za usemi zimetusaidia kuona namna namna akina dongo ana wenzake walivyokuwa katika harakati za kuikomboa nchi kutoka katika mikono ya wahujumu uchumi. Hata hivyo, matokeo ya utafiti yamebainisha kuwa mapambano dhidi ya uhujumu uchumi ni kitu kigumu ambacho kinahitaji wananchi pamoja na serikali yao kuungana na kuwa kitu kimoja. Sambamba na hilo pia elimu inatakiwa kutolewa kwa wananchi ili waweze kuelewa athari za uhujumu uchumi kwa maendeleo ya taifa na jamii kwa jumla. Watumishi wa umma wakiwemo mahakimu ambao hupindisha sheria baada ya

kupewa chochote kitu na wahujumu uchumi wachukuliwe hatua za kinidhamu ili kukomesha vitendo hivyo.

5.4 Mapendekezo

Utafiti wetu ulihusu kuchunguza mbinu za kisanaa katika tamthiliya ya *Morani*, utafiti kama huu unaweza kufanywa kwa kuangalia tamthiliya nyingine za Emmanuel Mbogo hasa zile alizoziandika katika miaka ya hivi karibuni.

Utafiti linganishi baina ya matumizi ya mbinu za kisanaa unaweza kufanywa kwa kulinganisha *Morani* na tamthiliya nyingine za Emmanuel Mbogo au mtunzi mwingine wa tamthiliya za Kiswahili.

MAREJELEO

Babbie, E. (1992). *The Practice of Social Research*. Calfonia: Wadsworth Publishing Company.

Babbie, E. (1999). *The Basics of Social Research*. Belmont: Wadsworth.

Barthes, R. (1994). *The Semiotic Challenge*. Berkely: University of Califonia Press.

Cobley, P. (2001). *The Routledge Companion to Semiotics and Linguistics*. London: Routledge.

Creswell, J. W. (2009). *Research Design: Qualitative and Mixed Methods Approaches*. Los Angeles: SAGE Publications.

Daniel, Z. (2012). "Ubwege katika Tamthilia ya *Amezidi*." Tasinifu ya Uzamili, Chuo Kikuu cha Dar es Salaam.

Eco, U. (1976). *A Theory of Semiotics*. Bloomington: Indiana University Press.

Good, G. V. (1966). *Essentials of Educational Research*. New York: Maridith Publications Co.

Hussein, E. (2003). "Hatua Mbalimbali za Kubuni na Kutunga Tamthiliya Kufuatana na Misingi ya Ki-Aristotle." Katika *Makala za Semina ya Kimataifa ya Waandishi wa Kiswahili 111 FASIHI*. TUKI: Dar es Salaam.

Kiango, S. D. (1992). "Taswira ya Mwanamke katika Tamthiliya za Kiswahili za Kenya Zilizochapishwa." katika *Baragumu Juzuu 1 na 2,* Tasinifu ya Uzamili, Chuo Kikuu cha Maseno.

King'ei, K. (1987). "Usanifu wa Lugha katika Uandishi wa E. Hussein." Katika *Mulika* Na. 19. TUKI: Dar es Salaam.

Kothari, C. R. (2008). *Reserch Methodogy: Methods and Techiniques*. New Delhi: New Age Internationl Publising Ltd.

Ligembe, N. E. G. (1995). “The Uses of Metaphor in Penina Muhando’s Lina Ubani.A Stylistic Analysis.” M.A Disertation, University of Dar es Salaam.

Magare, F. A. (2002). “Uhakiki wa Tamthiliya ya Amezidi kama Kazi ya Kibwege.” Tasinifu ya M.A Chuo Kikuu cha Nairobi.

Mark, G. (1995). *Postmodern Semiotics: Material Culture and the Forms of Postmodern Life*. Oxford: Basil Blackwell.

Masoud, S. (2013). “Maudhui na Fani katika Tamthliya za Kiswahili: Utafiti Linganishi wa Tamthiliya za Kivuli Kinaishi na Mashetani.” Tasinifu ya Uzamivu, Chuo Kikuu Huria cha Tanzania.

Mbogo, E. (1993). *Morani*. Dar es Salaam: Macmillan Aidan Ltd.

Mosoti, Z. M. (1993). “Maudhui katika Tamthiliya Nne za Emmanuel Mbogo.” Tasinifu ya M.A Chuo Kikuu cha Nairobi.

Mlama, P. O. (2003). “Utunzi wa Tamthiliya katika Mazingira ya Tanzania.” Katika *Makala ya Semina ya Kimataifa ya Waandishi wa Kiswahili III. Fasihi*: Dar es Salaam: TUKI.

Msokile, M. (1993). *Uchambuzi na Uhakiki: Karibu Ndani*. Dar es Salaam: DUP.

Mugambi, P.J.M. (1982). “Uhakiki wa Maudhui katika Tamthiliya za Kiswahili za Kenya Zilizochapishwa.” Tasinifu ya M.A Chuo Kikuu cha Nairobi.

Musyoka, F. M. (1996). “Uhakiki wa Fani katika Tamthiliya za Jay Kitsao.” Tasinifu ya Uzamili Chuo Kikuu cha Nairobi.

Mutembei, A. (2012). *Korasi katika Fasihi: Nadharia Mpya ya Uhakiki*. Dar es Salaam: TATAKI.

Nazarova, T. (1996). *Linguistics and Literary Semiotics*. Moscow: Moscow State University Press.

Nicholous, A. (2011). “Falsafa ya Ubuntu katika Tamthiliya za Penina Mhando.” Tasinifu ya Uzamili, Chuo Kikuu Cha Dar es Salaam.

Njogu, K. na Chimerah, C. (1999). *Ufudishaji wa Fasihi*: *Nadharia na Mbinu*. Nairobi: JKF.

Nyerere, J. K. (1967). *Ujamaa: The Basis of African Socialism*. Dar es Salaam: Tanganyika Standard.

Nyerere, J. K. (1977). *The Arusha Declaration Ten Years After*. Dar es Salaam: Government Printer.

Ramadhani, D. (2005). “The Uses of Metaphors in Mbogo’s *Ngoma ya Ng’wanamalundi* and Hussein’s *Mashetani*: A Stylistics Comparison.” M.A Thesis, UDSM.

Robson, C. (2007). *How to Do A Reserch Project*: A Guide for Undergraduate Students. Carton Victoria: Blackwell Publishing.

Ryanga, S. A. na Maina, R. W. (2012). *Muongozo wa Mustahiki Meya*. Nairobi: Mvule Afrika Publishers.

Sarara, M. M. (1997). “Maudhui katika Tamthiliya za S.A Mohamed.” Tasinifu ya Uzamili, Chuo Kikuu cha Nairobi.

Semzaba, E. (2003). *Tamthiliya ya Kiswahili*. Dar es Salaam: Chuo Kikuu Huria cha Tanzania.

Sengo, T. S. Y. M. (1973). “Dhima ya Fasihi kwa Maendeleo ya Jamii.” katika *Jarida la Kiswahili*, Dar es Salaam: TUKI.

Sengo, T. S. Y. M. (1987). *Fasihi Simulizi*. *Sekondari na Vyuo*: Dar es Salaam: Nyanza Publications Agency.

Sengo, T. S. Y. M. (2009). *Sengo na Fasihi za Kinchi*. Dar es Salaam: AKADEMIYA

Sengo, T. S. Y. M. na Kiango, S. D. (2012). *Hisiya Zetu*. Dar es Salaam: TUKI.

Senkoro, F. E. M. K. (1997). "The Significance of Journey Motif in Zanzibar Falk Tailes." PhD Thessis, University of Dar es Salaam.

Wafula, R. M. (1999). *Uhakiki wa Tamthiliya*: *Historia na Maendeleo Yake*. Nairobi: Jomo Kenyatta Foundation.

Wamitila, K. W. (2002). *Uhakiki wa Fasihi*: *Misingi na Vipengele Vyake*. Nairobi: Poenix Publisher Ltd.

Wamitila, K. W. (2008). *Kanzi ya Fasihi*: Misingi ya Uchanganuzi wa Fasihi. Nairobi: Vide – Muwa.

Young, P. V. (1984). *Scientific Social Surveys and Research*. Enalewood Chiffs: Prentice Hall. Inc

Yin, R. K. (1994). *Case Study Research: Design and Methods*. (2nd eds.) Thousand Oaks Calif: SAGE Publishers.